SUPA JACKPOT
TZS. 1,142,132,257
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Fundi** kizimbani dai la kuhujumu EFD, kuipa 'shoti' serikali mil. 954/-

UKURASA 7




UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Agosti 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581397
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Samia atoa maelekezo mapya uuzaji chakula nje

• **Wafugaji** Mbarali kulipwa fidia bilioni 26/- kupisha hifadhi; ruzuku ya mbolea... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akisikiliza maelezo ya mnufaika wa mpango wa kuwawezesha vijana kwenye mifugo (BBT life Mifugo), Rest Mgonja, kuhusu mafanikio waliyopata kutokana na mradi wa ufugaji wa ng'ombe wa kisasa, katika maonyesho ya wakulima Nanenane jijini Mbeya jana. Anayeshuhudia ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega. **Picha zaidi Uk. 18. PICHA: IKULU**



UKURASA 3

Waombolezaji wakiaga miili ya wanafamilia watatu waliofariki dunia kwa ajali ya gari, Sia, Diana na Norah Msuya wakati wa ibada iliyofanyika viwanja vya Gofu Lugalo, Dar es Salaam jana na kuzikwa kwenye makaburi ya Kondo Ununio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Chalamila aongoza mamia kuaga miili ya dada watatu

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### PM ATAKA VIJANA KUPEWA KIPAUMBELE KUENDELEZWA



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi na watalaamu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa waweke kipaumbele...

## Askofu Munga: Nimenusurika, niko salama

UKURASA 3

**MICHEZO** GAMONDI ATOA SABABU UGUMU AZAM LEO UK.24

**KATUNI** UK.6



Wachuuzi wakiwa wamepanga bidhaa zao kwenye eneo la waenda kwa miguu kando ya barabara katika kituo cha daladala cha Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia atoa maagizo mapya kuuza chakula nje ya nchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amepiga marufuku wakulima kuuza mazao moja kwa moja nje ya nchi na badala yake ameziagiza Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo kuandaa mfumo rasmi wa kuwezesha mazao kuuzwa nje ya nchi.

Rais Samia alitoa agizo hilo jana wakati akifunga Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima katika viwanja vya John Mwakangale jijini hapa.

Alisisitiza kuwa serikali haijafunga mipaka ya kuuza mazao nje ya nchi isipokuwa kinachohitajika ni utaratibu mzuri wa uuzaji wa mazao hayo nje ya nchi ambao utawanufaisha wakulima.

"Naagiza Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), andaeni mfumo wa kuuza mazao nje ya nchi ambao utawanufaisha wakulima wetu," alisema Dk. Samia.

Kwa sasa, alisema kuna wafanyabiashara kutoka nje ya nchi wanaoingia nchini na magari yao na kwenda moja kwa moja kununua mazao kwa wakulima vijijini na wengine wanatoa fedha kwa mawakala wao mpakani ili wakawanunulie kwa wakulima.

Alikemea mfumo huo na kwamba haukubaliki kwa sababu hauna udhibiti wa serikali na wakati mwingine hauwanufaishi wakulima kutokana na bei ambazo wananunulia mazao hayo.

Dk. Samia alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA) ili inunue mazao ya wananchi na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi wanapaswa kununua kutoka wakala huo katika utaratibu anaoamini utawanufaisha wakulima.

"Mheshimiwa waziri nimekupatia fedha nyingi mwaka huu kupitia NFRA, nataka NFRA ndiyo inunue mazao ya wakulima na kuyauza kwa wanaoyahitaji nje ya nchi, hivyo kuanzia sasa mkulima haruhusiwi kuuza mazao moja kwa moja nje ya nchi," alisema Dk. Samia.

Aliagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kulitumia vizuri eneo lililotengwa kwa ajili ya mifugo wilayani Chunya lenye ukubwa wa zaidi ya ekari milioni 1.5 kwa kuliwekea miundombinu rafiki yakiwamo malambo kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Katika hatua nyingine Rais Samia alisema serikali inakusudia kuwalipa fidia wananchi wanaotakiwa kuhama kupisha Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika wilaya ya Mbarali kuwa zinahitajika Sh. bilioni 26.

Rais Samia alitembelea mabanda mbalimbali ya maonesho ikiwamo Kampuni ya Uzalishaji na Usambazaji wa Mbolea (YARA) Tanzania na kuomba iendelee kusambaza mbolea bila wasiwasi kwa kuwa serikali italipa.

Mkurugenzi Mkuu wa YARA Tanzania, Winstone Odhiambo, alimwambia Rais Samia kuwa wameweza kukwepa tatizo la mlipuko wa Uviko-19 pamoja na vita ya Urusi na Ukraine kwa kuendelea kusambaza mbolea.

Alisema wamehakikisha Tanzania inajitegemea, inapata mbolea ya kutosha ili kupata usalama wa chakula na kuongeza uzalishaji kwenye mazao ya mkakati ambayo yatakuza uchumi.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema serikali imetenga Sh. bilioni 320 kwa ajili ya NFRA kununua mazao ya chakula kukabiliana na tatizo la njaa.

Fedha hizo zimesaidia kuwapatia wananchi soko la uhakika la mazao yao ambayo yananunuliwa kwa bei nzuri kuliko inayonunuliwa na wanunuzi wa kawaida.

Vilevile, alisema wizara hiyo imetenga bajeti kwa ajili ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji hasa skimu za umwagiliaji na kuchimba visima.

Serikali pia ina mpango wa kuchimba zaidi ya visima 60,000 nchi nzima kwa ajili ya programu maalumu ya umwagiliaji na kila kisima kitakuwa kinatumiwa na wakulima 16.

"Kuanzia Agosti 20, mwaka huu, vijana wetu wa mradi wa BBT wataanza kupewa maeneo yao ya kilimo hasa kwa kuanzia kule Dodoma, vijana watafungiwa mifumo yote ya umwagiliaji na watapatiwa hatimiliki," alisema Bashe.

Bashe alisema serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 200 kwa ajili ya mbolea ya ruzuku na bei ya pembejeo hizo itaendelea kuwa ya mwaka jana kati ya Sh. 60,000 na 70,000 kwa mfuko.

Alisema, Mkoa wa Ruvuma unaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka ukifuatiwa na Rukwa na Mbeya na mazao yasiyokuwa ya nafaka, Mkoa wa Kagera unaongoza ukifuatiwa na Kigoma, Mbeya ukishika nafasi ya tatu.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega alisema serikali imeanzisha mikakati maalumu ya kuboresha sekta ya mifugo kwa kuanzisha utaratibu wa kunenepesha mifugo badala ya ufugaji holela ambao tija yake ni ndogo.

Vilevile, wizara imeanza kushirikiana na wakuu wa mikoa kukabiliana na migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kuwaondoa wafugaji ambao wamevamia maeneo wasiyoruhusiwa hasa kwenye mashamba.

Mkoa wa Morogoro mpaka sasa unaendelea kuwaondoa wafugaji kwenye Bonde la Kilombero na kuwapeleka kwenye maeneo mengine ambako wamewaandalia mazingira rafiki ya kufugia.

Wizara hiyo imeanza mikakati ya kuifufua Kampuni ya Uvuvi la Taifa (TAFICO) ili kuboresha uvuvi kwenye Bahari Kuu na wanashirikiana na baadhi ya wadau.

Alisema kwa sasa serikali inakusudia kununua meli nne za uvuvi na serikali ya Japan imesaidia kununua meli moja na kujenga majengo maalumu yenye baridi ya kuhifadhia mazao.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Makongoro Nyerere, aliiomba serikali kuongeza wigo wa upatikanaji wa mbolea ya ruzuku hasa maeneo ya vijijini ili iwafikie wakulima kirahisi.

Aliomba mbolea hizo zipatikane kuanzia ngazi za kata kutokana na sasa kupatikana zaidi maeneo ya mjini hasa kwenye makao makuu ya wilaya.

Vilevile, aliomba mbolea hizo ziwe zinapatikana kwenye vipimo vidogo badala ya kilo 50 kiwango ambacho baadhi ya wakulima wenye mashamba madogo hawakihitaji.

## ...Aagiza kufanyike tathmini matokeo mbolea ya ruzuku

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

RAIS Samia Suluhu (pichani chini) ameagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kufanya tathmini ya matokeo ya mbolea ya ruzuku iliyotolewa na serikali kwa wakulima nchini ili kuona kama imeleta mafanikio katika sekta ya kilimo.

Aliagiza hayo alipotembelea Kijiji cha Mbolea cha TFRA katika Maonesho ya Nanenane jijini Mbeya jana.

Rais alisema pamoja na kuwapo sekta zingine ikiwamo madini, kilimo ndicho kitakachokomboa nchi na serikali imeamua kutoa ruzuku ya mbolea ili kuongeza tija katika kilimo.

Alisema wakati serikali inaendelea kutoa ruzuku hiyo ya mbolea, ni muhimu TFRA kuanza kufanya tathmini ya kina kuhusu ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali, kuona kama inaleta manufaa kwa wakulima.

Rais Samia pia ameagiza TRFA kuimarisha na kuongeza kasi ya usambazaji wa mbolea ili iwafikie wakulima kwa haraka na wakati hasa katika kipindi cha msimu wa kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu agizo hilo la Rais, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephani Ngailo, alisema "...tumelipokea na tumeshaanza kulifanyia kazi ikiwamo kuongeza idadi ya mawakala katika kila kata pamoja na kutumia maghala ya vijiji ili usambazaji wa mbolea uwe wa haraka na kumfikia mkulima kwa wakati.

"Ni sahihi kabisa kufanya tathmini, tunatakiwa kufanya hivyo ili kujua nini mchango wa mbolea ya ruzuku katika kilimo nchini."

Mkurugenzi huyo alisema watafanya tathmini mara moja kwa kushirikiana na kitengo cha Wizara ya Kilimo kinachohusika na tathmini ya chakula na wachumi ili kujua nini mchango wa ruzuku katika kukuza uchumi.



# Askofu Munga: Nimenusurika, niko salama

**Na Maulid Mmbaga**

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Mashariki (DKMs) mkoani Tanga, Dk. Stephen Munga, amenusurika katika ajali mbaya ya gari.

Ajali hiyo ilitokea juzi Handeni mkoani Tanga alipokuwa akitoka Mkata kwenda Tanga baada ya gari alilokuwa akisafiria kupinduka na kuserereka hatimaye kuingia kwenye mtaro mrefu likiwa kwenye kasi. Kwa mujibu wa taarifa aliyoitoa jana, kwenye gari alikuwa na mkewe, Dk. Anneth Munga, pamoja na rafiki yao ambaye ni mwalimu wa elimu maalum. Askofu Dk. Munga na wenzake walikuwa wanatoka kwenye kikao na wadau wanaoshirikiana nao katika kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum.

Akielezea tukio hilo, Askofu Munga alisema aliona kwa macho yake misukosuko yote ndani ya gari ambalo lilibiruzika kwa zaidi ya mita 100 likipanda gema upande mmoja na kurushwa eneo lingine mara kadhaa.

"Wakati hayo yote yanatokea kwa mara nyingine maishani mwangu nilijikabidhi mikononi mwa Bwana (Mungu) nikijua sasa bila shaka ni mwisho. Sina maelezo ni kwa jinsi gani tumepona bila hata michubuko.

"Sasa najua kabisa kwamba huwa nasafiri na malaika wa Bwana kwenye gari. Baada ya misukosuko yote na gari kutulia nikamtazama mke wangu ambaye tulikuwa tumeshikana mikono wakati wote nikaona ni mzima," alisema.

"Nikageuka nyuma kumtazama na kumsemesha mwalimu nikajua ni mzima. Tukatoka nje ya gari ndipo baada ya muda mfupi watu wakatokea. Kila mtu aliyekuja alikuwa na msaada mkubwa kwetu," aliongeza.

Pia alisema, baada ya kutulia alipita mtu aliyemwita ustadhi akiwa na lori lake na ndiye aliyelivuta gari lao kutoka mtaroni bila gharama yoyote huku akimshukuru kwa wema huo pamoja na watu wote wakiwamo baadhi ya walimu wa shule iliyokuwa karibu na eneo walipopata ajali.

Askofu Munga pia alisema baada ya kupatwa na matatizo, walifika watu wengi na askari wa usalama barabarani kwa ajili ya kuwapatia msaada huku akibainisha kuwa askari waliofika eneo la tukio walikuwa watu wema na waliwasaidia isivyotamkika.

"Kuna watu kwa nyakati tofauti walikuwahi kuniambia kuwa huyo Mungu wako anakupenda sana usije ukamwacha. Amenikumbusha tena kuwa wakati wowote anaweza kunipumzisha lakini kwa sasa bado sijamaliza kazi yake. Ni kweli Mungu wetu anatisha hana mfano," alisema.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian la Uamsho, Emmaus Mwamakula, katika ukurasa wake wa Facebook alisema Askofu Munga amepona katika ajali ambayo nusura itwae maisha yake, mke wake na rafiki yao. Mwamakula alisema wanapomshukuru Mungu kwa ajili ya maisha yao wanapenda pia kuambatanisha ushuhuda wake ili watu wausome.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akifanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Uganda, Jessica Alupo, katika mkutano wa pili wa wakuu wa nchi na serikali wa nchi 25 za Afrika, wanachama wazalishaji wa zao la kahawa jijini Kampala, Uganda jana. **PICHA: OMR**

# Chalamila aongoza mamia kuaga miili ya dada watatu

**Na Romana Mallya**

WAKATI mamia ya watu walijitokeza jana katika kuaga miili ya dada watatu wa familia moja waliofariki dunia katika ajali pamoja na kaka yao, kanisa limetoa neno la faraja kwa wazazi wao kutoka Kitabu cha Ayubu.

Waliofariki katika ajali hiyo iliyotokea Agosti 2, mwaka huu, ni Nechi Msuya, ambaye alizikwa Agosti 6, mwaka huu, kijijini kwao Msangeni Ugweno, Mwanga, mkoani Kilimanjaro na dada zake watatu, Dk. Norah, Sia na Diana.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, aliongoza mamia ya watu hao katika ibada ya kuaga miili mitatu iliofanyika viwanja vya Gofu, Kawe na baadaye kuzikwa katika makaburi ya Kondo Ununio, Dar es Salaam.

Msaidizi wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Mchungaji Chediel Lwiza, akiongoza ibada hiyo jana kwa niaba ya Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Alex Malalusa, alisema misiba ya namna hiyo si myepesi.

Alisema neno la faraja ni kutoka kitabu cha Ayubu 1:22 unaosema, "Katika mambo hayo yote Ayubu hakufanya dhambi wala, hakumwazia Mungu kwa upumbavu."

Mchungaji Lwiza alisema: "Misiba ya namna hii si myepesi. Na misiba inayotokea mara moja wakati mmoja siku moja eneo moja tukio moja, inaumiza na huwa inaacha maswali mengi.

"Sisi tukisoma tunafundishwa kuna misiba ya aina saba. Mara nyingi sisi Wakristo na walio wengi pia huwa tunaangalia mtu amekufaje, kimsingi tuna misiba takribani saba.

"Kitabu cha Ayubu, ambaye kiasili kabisa sifa ya Ayubu, imani ya Ayubu, tabia ya Ayubu, maisha ya Ayubu ya siku kwa siku, ukisoma sura ya kwanza hayaelezwi na mwanadamu, hayaelezwi na baba yake wala mama yake, hayaelezwi na mjomba wake wala binamu wake, sifa ya Ayubu inaelezwa na Mungu mwenyewe," alisema.

Alisema sehemu ya kwanza Mungu anayataja maisha ya imani na kiroho ya Ayubu na ya pili, inaeleza maisha ya kawaida ya siku kwa siku na ile ya tatu inamtaja kama baba wa familia, ikiwamo idadi ya watoto wake na sifa zao zinatajwa.

"Anayetaja hivyo ni Mungu. Tulitegemea katika hali ya kawaida, ikiwa Mungu anaweza kutujua kwa kiwango hicho, sisi labda tungefikiri tusingeguswa na chochote, tusingepata shida yoyote, inawezekana kama Mungu angetujua kwa namna hiyo, hata wanadamu wangetuogopa, hata marafiki wangetuheshimu zaidi," alisema.

Alisema lakini wanapata kitu cha tofauti kwamba namna Mungu anavyowafahamu na kuwajua, wakati mwingine ni njia ya kupima imani na maisha yetu.

"Nikuambie baba yangu Msuya na mama yangu Msuya, jinsi ulivyowafahamu watoto wako, ukawabatiza kwenye Usharika wa Majengo pale Moshi, Kilimanjaro. Jinsi mlivyowafahamu Nechi, Sia, Diana na Nora, Mungu aliwajua zaidi yenu.

"Aliwatambua namna ambavyo mfumo wa maisha yao kwenu kwa ndugu kwa familia. Mungu alijua zaidi, huyu ndugu anayeitwa Ayubu, alipata misiba mitatu na si rahisi kwa mwanadamu mwenye mwili wa nyama na damu kwa wakati mmoja kupata misiba mitatu kwa wakati mmoja, siyo kitu chepesi.

"Msiba wa kwanza ni mifugo yake yote, msiba wa pili wafanyakazi wake wote, msiba wa tatu watoto wake wote, kana kwamba haitoshi wakaanza kushughulika na afya yake (Ayubu) hata rafiki zake wakamkimbia.

"Dada zetu watatu leo tunawaaga tunakwenda kuwazika. Kaka yetu mmoja tayari tumeshamzika, walikuwa wanakwenda Ugweno, Msangeni kwenye msiba. Hawakuwa wanakwenda kwenye starehe, walikuwa wanakwenda kufariji, wakaitwa wote. Ayubu msiba yake yote na kufunga kwake kote, kipekee alitoa sadaka kwa watoto wake, Mungu akawachukua.

"Sia huyu alikuwa anakuja ofisini kwangu anasema nakuja kwako kama Mchungaji, kama kaka, ninamuuliza nini ananiambia 'NSSF (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) za wachungaji sijaziona. Naomba NSSF za wachungaji,' ananiambia 'Kaka mwezi huu usipite' na mimi ninamwambia, Sia tutajitahidi mwezi huu usipite," alisimulia.

Mchungaji Lwiza alisema waliposikia Sia ambaye aliyeguswa na maisha ya wachungaji amelala. Wampate wapi mwingine anayeshughulika na maisha yao baada ya kustaafu.

**KAULI YA RC**

Akizungumza katika ibada hiyo akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, Chalamila alisema: "Rais Samia yupo pamoja na sisi na jambo kubwa alilozungumza, ameumizwa sana na aliniambia "Ninaumizwa sana ninapokuta wanawake wenzangu tena katika umri huu, wasomi na wanaotegemewa kupoteza maisha yao." Na mimi nimeamua nije kulisema hili kwenu kwamba Mheshimiwa Rais ameguswa kiasi cha kutosha.

"Hapa tunaye mtumishi wake mmoja anayetoka kwenye ofisi yake na ameahidi kwamba kwa siku ya kesho (leo) familia zote tatu watazipitia tukiwa pamoja na kuzipa neno au mkono wa pole.

"Kwa hiyo kesho familia ya Mzee Msuya mtatupokea ili tuje tuzungumze na familia kwa ujumla wake, lakini kwa neno ambalo Mheshimiwa Rais ambalo ametuachia," alisema.

Chalamila alisema Rais Samia amemwagiza azungumze na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na wa Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI) kuwa wazazi hao walipoteza watoto wanne, watibiwe kwa hadhi maalum (VIP) na pia kwa mikoa ambayo wazazi watakuwapo, wakuu wa mikoa hiyo wahakikishe hawapati mnyororo mpana wa kusumbuka.

Mkurugenzi Mkuu NSSF, Masha Mshomba, alitoa pole kwa familia na kuomba watu waendelee kuziombea familia hizo ambazo kwa sasa zinahitaji neno la faraja ili kuvuka katika kipindi kigumu.

Alisema Sia alikuwa mtumishi mwenzao ambaye aliajiriwa ndani ya shirika hilo tangu miaka ya tisini na alipenda kazi na kuwapenda wenzake na kupenda kuiona NSSF inakwenda mbele.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Dk. Yahya Nawanda, akizungumza kwa niaba ya wenzake waliowahi kusoma chuo kimoja na Dk. Norah, Afrika Kusini, alisema wamefika hapo kusherehekea maisha yake na kwamba enzi za uhai wake alipenda kuinua wengine, kusoma na kuandika machapisho mbalimbali.

"Kupitia yeye (Dk. Norah) ametoa PhD nyingi. Tumekubaliana tutamuenzi Dk. Norah kwa kuandika kitabu. Hicho kitabu nitakifadhili mimi. Tuliishi naye zaidi ya miaka mitano ndiye alikuwa mwanafunzi maarufu Durban, Afrika Kusini kuliko yeyote yule, hata kazi za kufundisha alituunganisha yeye," alisema.

# Samia avutiwa bima ya kilimo

**Na Mary Geofrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameitaja huduma ya bima ya kilimo inayotolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kama moja ya suluhisho muhimu katika kuwahakikishia wakulima kipato cha uhakika.

Vilevile, amewataka wito kwa wakulima nchini kutumia vyema huduma mbalimbali za kibenki zinazotolewa na serikali na taasisi za kifedha kuboresha kasi ya ukuaji wa sekta hiyo.

Rais Samia alitoa wito jana alipotembelea banda la NBC katika Maonesho ya Kilimo ya Nanenane jijini Mbeya baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, kuhusiana na fidia yenye thamani ya dola za Marekani 33,537.89 sawa na Sh. milioni 85 iliyotolewa na benki hiyo kwa wakulima wa tumbaku walioathirika na mvua za mawe katika msimu wa kilimo uliopita.

Kwa mujibu wa Rais Samia, serikali na taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya NBC, zimejitahidi kubuni huduma mbalimbali zinazolenga kuwawezesha wakulima ikiwamo mikopo ya fedha na zana za kilimo, hivyo ujio wa huduma ya bima ya kilimo utasaidia kuwahakikishia wakulima kipato cha uhakika kutokana na shughuli zao badala ya kubahatisha kama ilivyokuwa awali.

"Ndugu zangu wakulima mnataka mmepewe nini tena? Kwa sasa mnawezeshwa kwenye kila hatua ikiwamo pembejeo bora, zana za kilimo za kisasa na mikopo mbalimbali. Pamoja na vyote hivyo, changamoto ilikuwa imebaki kwenye hasara zitokanazo na majanga mbalimbali ikiwamo mafuriko na mvua za mawe.

"NBC wamekuja na huduma ya bima ya kilimo ili kumaliza tatizo hilo ili kuwahakikishia uhakika wa mapato yenu, bado mnataka mpewe nini tena?" Rais alihoji.

Alisisitiza taasisi za kifedha kuhakikisha zinaendelea kushusha riba zao ili kuwavutia zaidi wakulima watumie huduma za kifedha kutoka taasisi hizo kwa faida zaidi.

Akifafanua zaidi kuhusu huduma ya Bima ya Kilimo inayotolewa na Benki ya NBC kwa kushirikiana Kampuni ya Bima ya Jubilee, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema itasaidia kuondoa changamoto ya hasara walizokuwa wakizipata wakulima kutokana na majanga mbalimbali yaliyo nje ya uwezo wao ikiwamo mafuriko, moto na mvua za mawe ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikiathiri ustawi wa wakulima na kusababisha baadhi yao kuwa na hofu kuwekeza katika sekta hiyo muhimu.

"Rais hatua hii ya NBC ni mwanzo wa kuelekea katika utekelezaji mkubwa zaidi wa pamoja katika kuhakikisha kwamba huduma hii ya bima ya kilimo inawafikia wakulima wengi zaidi... hivyo ninawapongeza sana NBC kwa kuanzisha hili,'" alipongeza Bashe.

Awali akizungumza mbele ya Rais Samia, Sabi alisema malipo yatokanayo na bima ya kilimo ya benki hiyo ni mwendelezo kwa kuwa tayari benki hiyo ilikwishatoa fidia ya dola za marekani 4,000 (Sh. milioni 10) kwa mwaka wa kwanza wa uendeshaji wa huduma hiyo huku akitaja mikoa ambayo wakulima wake wamenufaika na bima hiyo kwa msimu wa pili kuwa ni Tabora, Geita na Shinyanga ambapo jumla ya vyama vya msingi (AMCOS) 10 vimenufaika na malipo hayo.

"Malipo haya yanahusisha jumla ya wakulima 140 kutoka AMCOS 10 za mikoa ya Tabora, Geita na Shinyanga ambao mazao yao ya tumbaku yaliathirika vibaya na mvua za mawe; eneo la ekari 2,531 liliathirika kwa viwango tofauti na kuathiri mavuno yao.

"Kupitia Bima ya Kilimo ya NBC inayoendeshwa kwa ushirikiano na Kampuni ya Bima ya Jubilee waathirika hawa wamelipwa fidia," alisema Sabi huku akitoa wito kwa wakulima wa mazao mbalimbali kuchangamkia bima hiyo.



Mtoa huduma ya afya ngazi ya jamii Kata ya Kipunguni, Joyce Temba, akitoa elimu kuhusu mzazi anavyotakiwa kumbeba mtoto na kumnyonyesha katika mafunzo yaliyoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# ACT yamulika vikwazo kwa wakulima

**Na Abeid Makarabo**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeadhimisha Nanenane mwaka huu kwa kuziangazia changamoto zinazowakabili wakulima, kikishauri hatua za makusudi zichukuliwe kuzitatua.

Taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Msemaji wa Sekta ya Kilimo, Umwagiliaji na Maendeleo ya Ushirika wa chama hicho, Mtutura Abdallah, ilibainisha baadhi ya changamoto wanazokumbana nazo wakulima nchini zinajumuisha uporaji wa ardhi ya wakulima kwa kigezo cha uwekezaji katika kilimo.

Katika taarifa yake hiyo, Abdallah alitaja changamoto nyingine kama vile tishio la uhuru wa wakulima katika uzalishaji, uhifadhi wa mbegu na mazao ya kilimo kupitia dhana ya kilimo biashara na kuwapo tija ndogo katika uzalishaji kunakosababishwa na matumizi hafifu ya teknolojia ya wakulima wenyewe.

Alisema chama chao kinapendekeza hatua za makusudi zichukuliwe na serikali kukabiliana na changamoto hizo na kuleta mapinduzi katika kilimo, kwa kutambua mchango wa kilimo katika uchumi wa nchi.

"Haiwezekani nchi hii taswira ya umaskini iwe ni mkulima. Ni lazima hatua za makusudi zichukuliwe kwa ajili ya kufanya mapinduzi katika kilimo kwa kufungamanisha sekta ya kilimo na viwanda," alisema.

Alizitaja hatua hizo ni pamoja na serikali kuongeza jitihada za kulinda uhuru wa wakulima katika uzalishaji na soko la mazao ya kilimo kwa kuhakikisha uhifadhi, uzalishaji na usambazaji wa mbegu asili, matumizi ya mbinu za kilimo cha kioganiki kwa kutumia ujuzi asilia na kuachana na matumizi ya dawa za viwandani ambazo huathiri mazingira.

Pia aliitaka serikali kuwahakikishia wakulima upatikanaji, umiliki na matumizi ya ardhi ya kijiji kwa madhumuni ya kukidhi haja ya kijamii, viwanda vidogo maeneo ya vijijini vinavyoendeshwa, kumilikiwa na kusimamiwa na wakulima wenyewe kupitia vyama vyao vya ushirika ambavyo vitaweza kuzalisha ajira na kuchakata mazao.

# Kamati yaita wadau marekebisho sheria, imo bandari

**Na Mwandishi Wetu**, DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imewaita wadau kutoa maoni yao kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2023 unaohusu masuala kadhaa ikiwamo bandari.

Muswada huo, mbali na mambo mengine, unapendekeza marekebisho ya sheria ya mamlaka ya nchi kuhusiana na umiliki wa mali na rasilimali asilia, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria hizo hauathiri utendaji wa maeneo ya bandari, bandari za nchi kavu na bandari za maeneo ya maziwa nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa cha Ofisi ya Bunge, kamati hiyo inawaalika wadau wote wenye maoni kuhusu muswada huo kufika kutoa maoni yao katika ofisi hiyo, pia kwa kutuma kwa njia ya posta au barua pepe.

Muswada huo ambao ulisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa 11 wa Bunge unalenga kuwezesha bandari katika Jamhuri ya Muungano kufikia viwango vya kimataifa vya kiutendaji na kuvutia nchi nyingi zaidi na shehena kubwa za mizigo kutumia bandari za nchini.

Muswada pia unapendekeza kurekebisha Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159 kwa lengo la kuweka masharti bora ya utekelezaji wa sheria hiyo, ikiwamo kurekebishwa kwa kuboresha majukumu ya shirika ili kuruhusu kufanya shughuli zake ambazo zinaendana na maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu uliopo na unaoendelea kutokea duniani.

Pia, majukumu ya shirika yanarekebishwa ili kuondoa mgongano kati ya majukumu ya shirika na taasisi nyingine na kuweka mkazo katika utafiti wa viwanda kwa kuwa utafiti wa kiteknolojia unashughulikiwa chini ya utafiti wa kiviwanda.

Kadhalika, muswada huo unapendekeza kurekebisha Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188 kwenye kifungu cha nne. Kinarekebishwa ili kushusha viwango vya msamaha.

Lengo la marekebisho ni kuongeza ulinzi na usalama kwa wafanyakazi, umma na mazingira kutokana na mmuliko wa mionzi unaotokana na madini yanayotoa mionzi na viasili vya mionzi vinavyotokana na asili (NORMs) na kufuata viwango vya usalama vinavyokubalika kimataifa.

Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha katazo linalozuia kushughulika na madini yanayotoa mionzi bila ya kuwa na leseni au kusajiliwa kwa ajili hiyo ili kuhakikisha ulinzi na usalama katika kushughulika na vyanzo vya mionzi.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiangalia kiatu kilichotengenezwa na kiwanda cha wajasiriamali cha Faru Products jijini Dodoma, kabla ya kufungua kongamano la vijana la mkoa huo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Katibu Mkuu wa TUICO agonga mwamba kortini kesi ya kashfa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Ilala, imetupilia mbali ombi la Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Boniface Nkakatisi, la kutaka mwanachama Mambo Mkufu kulipa Sh. milioni 200 kwa madai ya kumkashfu.

Kutokana na kushindwa kesi hiyo, Nkakatisi ametakiwa kulipa gharama za kesi hiyo. Nkakatisi alikimbilia mahakamani, kumshtaki Mkufu, aliyekuwa Mwenyekiti wa TUICO Tawi la Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mikocheni kwa madai kuwa aliandika barua ya kumkashifu na aliandaa mkutano wa waandishi wa habari na kumdhalilisha.

Akitoa uamuzi katika kesi ya madai ya kashfa namba 79 ya mwaka 2021, Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rehema Lyana, alisema mlalamikaji hakupeleka ushahidi wowote wa kuthibitisha madai hayo.

Pia alisema hakuna ushahidi unaoonyesha au kuthibitisha mlalamikaji alivyoteseka ili kuiwezesha mahakama kumpatia hasara ya jumla kama ilivyoombwa.

"Zaidi ya hayo, ili udhalilishaji huo usimame maneno yanayolalamikiwa lazima yafafanuliwe kwa uthabiti na lazima yawe ndani ya maana yake yawe ya kukashfiwa,"alisema Hakimu Lyana.

Hakimu Lyana pia alisema kupitia barua hiyo hakuna mahali inayoonesha kuwa Mkufu alimkashfu mlalamikaji kwenye vyombo vya habari, kwenye ofisi, vyombo vya usalama na magazeti.

Kwa mujibu wa hakimu, katika kesi ya kashfa, mlalamikaji lazima athibitishe vipengele muhimu vifuatavyo, kwanza, kauli inayolalamikiwa kama ni ya kumkashifu, pili, kwamba ilichapishwa, yaani mawasiliano kwa mtu wa tatu.

Alisema kipengele cha tatu ni uongo, nne, taarifa hiyo ilikuwa na madhara kwa sifa ya mdai na tano, kwamba taarifa hiyo haikuwa ya upendeleo na katika kesi hiyo ilikuwa haina vipengele hivyo.

" Kesi ya mlalamikaji haina vigezo muhimu kwa kosa la kashfa kusimama, kwa hiyo ninaitupilia mbali kwa gharama," alisema.

Katika hati ya madai, Nkakatisi alidai kuwa Mkufu ambaye ni mwanachama wa TUICO kutokana na ajira yake TANESCO, Julai 19, 2021 kwa nia ovu na bila kuwa na sababu halali, alisababisha kuchapishwa kwa maneno yenye kashfa dhidi yake.

Nkakatisi ambaye anawakilishwa na Wakili Mathew Kabunga pia alidai kuwa Mkufu alisababisha kusambazwa kwa barua yake barua yenye maneno ya kashfa dhidi yake ya Julai 19, 2021.

Pia alidai kuwa katika barua hiyo ambayo Mkufu alimwandikia yeye kama Katibu Mkuu wa TUICO, alimshambulia binafsi kwa jina lake kwa kusudi la kumharibia hadhi yake kutokana na kile anachokiita maelezo ya uongo.

# PM ataka vijana kupewa kipaumbele kuendelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi na wataalamu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa waweke kipaumbele kuendeleza vijana ili washiriki kikamilifu katika shughuli za kuinua uchumi na kuwapatia ujuzi na mbinu za ujasiriamali.

Pia Majaliwa alisisitiza kila mkoa uandae mpango mahususi wa kuhamasisha vijana kufanya shughuli zenye staha na kuwavutia wengi kushiriki shughuli za kiuchumi, Mkoa wa Dodoma umeanza na mingine ijiandae.

Alitoa wito huo jana wakati akifunga kongamano la vijana na kuagiza wapatiwe mbinu na ujuzi wa ujasiriamali ili wachangamkie fursa zilizopo mbele yao.

Alizitaka taasisi na mifuko ya uwezeshaji kwa vijana zitangaze fursa zilizopo na watumie mbinu mbalimbali zikiwamo redio hasa za kijamii kuwafikia walengwa.

"Kila mmoja kwa nafasi yake ashiriki katika kuwapa taarifa kuwaongoza na kuwaunganisha na fursa mbalimbali za kukuza mitaji yao.

"Halmashauri zihakikishe kuwa vijana walio tayari kufanya uwekezaji katika shughuli za uchumi wanapata taarifa za fursa za mitaji. Nyote mlimsikia Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisisitiza kuhusu kutoa taarifa kwa walengwa," aliagiza.

Alisema mikoa iandae utaratibu wa kutoa elimu wapate stadi za maisha na kufanya maamuzi sahihi ya utunzaji wa mazingira na mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi, maadili, uzalendo, mapambano dhidi ya dawa za kulevya na rushwa.

Majaliwa alisema vijana wote walioshiriki katika kongamano hilo anaamini wameshaiva na wako tayari kwa kazi na kuwataka watumie maarifa waliyoyapata kuchangamkia fursa ndani na nje ya Mkoa wa Dodoma. Vilevile, wawe wadadisi kubaini na kuchangamkia fursa hizo.

"Mmeshapata maarifa mengi kupita kongamano hili wakati umefika sasa mnakwenda kutumia maarifa hayo kwa vitendo. Mikoa nayo iandae utaratibu wa kutoa elimu kuhusu masuala muhimu na mahsusi ya mtambuka kwa vijana ili wapate stadi za maisha na kufanya maamuzi sahihi."

"Nitoe wito kwenu vijana kuitumia fursa hii muhimu na adhimu mliyoipata katika kongamano hili kuanzisha na kuendeleza miradi yenu na baadaye kuondoa tatizo la ajira na umaskini kwa nchi yetu. Muhimu ni kuthubutu, kuchukua hatua, kuanza kidogo na kukua. Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ana dhamira njema kuhusu ustawi wa vijana."

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233 S.L.P.
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba, 2888, 40470DODOMA,

08.08.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe 10-08-2023 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili:

**T773 EAP / T 887DJB / T112EAG/ T 578EAZ**

Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 21.00 / Upana - mita 4.80 / Kimo - mita 4.90**

2. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi, S.L.P. 2888, 40470DODOMA,

08.08.2023

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 11.08.2023 mnatangaziwa hadi 25.08.2023 kampuni ya CEVA Interfreight itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya Dar Es Salaam kuelekea Mzenga, gari hilo lenye namba za usajili

**NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo: Urefu - Mita 36.0
**Upana - Mita 7.50**
**Kimo - Mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro mpaka Mlandizi,** magari yatasafiri muda wa usiku **( Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)**. Kutoka **Mlandizi** kwenda **Mzenga** magari yatasafiri muda wa mchana **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nanenane itumike kuleta mageuzi ya kiuchumi

**WATANZANIA** jana waliadhimisha Sikukuu ya Wakulima maarufu Nanenane ambayo kitaifa ilifanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya. Licha ya kufanyika kitaifa, maadhimisho hayo pia yalifanyika katika maeneo mbalimbali kama vile Lindi, Arusha, Morogoro, Dodoma, Tabora na Mwanza katika ngazi ya kanda.

Maadhimisho hayo ambayo huambatana na maonyesho mbalimbali ya kilimo, mifugo na uvuvi, hufanyika kwa lengo la kuonyesha kazi mbalimbali zinazofanywa na wadau wa sekta hizo pamoja na utafiti na ugunduzi wa teknolojia mbalimbali katika maeneo hayo. Pia taasisi mbalimbali kama benki na mifuko ya hifadhi ya jamii hushiriki katika maadhimisho ya Nanenane kwa ajili ya kutoa elimu na huduma zinazohusu shughuli zao.

Katika wiki ya maadhimisho hayo, viongozi mbalimbali walioko madarakani na wale wastaafu hupata fursa ya kutembelea mabanda ya taasisi zinazohusika na kilimo, mifugo na uvuvi na kutoa matamko mbalimbali. Miongoni mwa maagizo ambayo yamekuwa yakitolewa ni kuhusu uboreshaji wa shughuli zinazohusu sekta hizo na pia kusisitiza uzalishaji wenye tija kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Kwa hakika, Nanenane ni fursa au jukwaa kwa ajili ya wakulima, wafugaji na wavuvi kupata ujuzi na elimu itakayowasaidia kujiunga na shughuli hizo kwa ajili ya kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja, familia na jamii. Kwa maneno mengine, maonyesho hayo yamesababisha baadhi ya watu kubadilisha fikra katika maisha yao na kuachana na ajira na kufanya shughuli za ufugaji na hatimaye maisha yao kuwa bora tofauti na walipokuwa wakifanya shughuli zingine zikiwamo ajira.

Iko mifano ya watu waliofanikiwa katika hilo akiwamo mwanasiasa mmoja aliyekuwa mbunge kwa takribani miaka 10. Mwanasiasa huyo amekuwa akitoa ushuhuda mara kwa mara kwamba alipojifunza kuhusu ufugaji wa samaki, aliamua kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi kuhusu tasnia hiyo katika Chuo cha Uvuvi Mbegani, Bagamoyo na sasa ana mafanikio makubwa kutokana na kazi hiyo. Katika ushuhuda wake, amekuwa akisema wazi kwamba laiti angejikita katika shughuli hiyo kabla ya hivi sasa angekuwa bilionea lakini hajutii kuchelewa kuanza.

Kwa kutumia mfano huo, wako watu waliobadilisha mtazamo kuhusu maisha kwa kuingia katika shughuli za uzalishaji kwenye maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kwa mantiki hiyo, elimu inayotolewa katika maonyesho ya Nanenane ni fursa kubwa kwa Watanzania wengi kubadilika kifikra na kujiingiza katika uzalishaji na hatimaye kupata mafanikio kuliko kuendelea kufikiria kufanya kazi za ofisini pekee.


Ni wakati mwafaka sasa Nanenane iliyomalizika jana ilete mageuzi katika kilimo, mifugo na uvuvi ili kuleta tija katika uchumi wa nchi. Elimu iliyopatikana katika sherehe hizo itumike kwa wakulima katika kuleta mageuzi ya sekta hizo hasa katika kutumia utaalamu kwenye uzalishaji.

Hivi sasa kwa mfano, kuna taarifa za kuwapo upungufu wa mafuta ya kupikia hatua ambayo hulilazimu taifa kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi. Kwa mantiki hiyo, wakulima, taasisi na kampuni zinazojihusisha na sekta hiyo, wanapaswa kuelekeza nguvu katika kuhakikisha pengo la bidhaa hiyo linapungua au kumalizika kabisa.

Aidha, kama Rais Samia Suluhu Hassan alivyosisitiza jana kuhusu masoko ya nyama nje ya nchi, Watanzania wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo kwa kufuga mbuzi na ng'ombe kwa wiki ili kupata bidhaa ya kutosha kutosheleza mahitaji katika nchi mbalimbali. Mambo hayo yanawezekana kama kutakuwa na jitihada za makusudi na utashi wa kisiasa katika kuendeleza sekta hizo na kuleta mageuzi ya kiuchumi nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Umma ufunzwe kubaini 'mchwa'

**KATIKA** jitihada za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo uboreshaji wa huduma za jamii na kukuza uchumi, kuanzia vijijini hadi mijini, kufuja fedha za umma kumekuwa ajenda ya wakati wote.

Utasikia barabara imejengwa chini ya kiwango, fedha za ujenzi wa mradi huu hazijulikani zilipo na madai kuwa pesa zimetumika bila risiti wala hazifahamiki ziko wapi ni ya kawaida.

Ni mambo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan, anayakemea na kutaka anayebainika kuhusika achukuliwe hatua za kisheria. Kuwapo kwa vitendo hivyo, vya ufujaji wa fedha za miradi katika maeneo mbalimbali, kinaleta ujumbe kuwa ni wazi nchi haiwezi kupiga hatua kwenda mbele, badala yake inazidi kurudi nyuma.

Ninadhani umefika wakati sasa wananchi kujengewa uwezo ili wawe wanafuatilia fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo kwenye maeneo yao, wajue ni kiasi gani, kwa ajili ya miradi gani na zinatumikaje.

Hatua hiyo inawasaidia kujua utekelezaji wa miradi kama unalingana na kiasi cha fedha kilichotumika, ili kama watabaini kuwapo kwa 'madudu', basi wafikishe taarifa kwa vyombo husika ikiwamo TAKUKURU. Ninaamini mafunzo ya ufuatiliaji wa fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo, inayofanyika maeneo mbalimbali, yanaweza kuwa msaada kwa wananchi kuelewa umuhimu wa ufuatiliaji wa miradi hiyo.

Mafunzo yanaweza kuwafanya wananchi na kuwa makini kwa kufuatilia hatua kwa hatua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ili pale wanapobaini kasoro wawe tayari kuzitolea taarifa haraka.

Kupitia mafunzo, wananchi wanatakiwa kujua fedha za ujenzi wa majengo ya umma, barabara na miradi mingine, ziwe wazi, kuanzia siku ya kwanza ya kutangaza zabuni pamoja na ufunguzi wake. Ninaamini wananchi wakielimishwa, na kupewa fursa ya kuchagua miradi waitakayo na kushirikishwa pia kuwapo kwa kumbukumbu za ujenzi na matumizi katika kila eneo, hatua hiyo inaweza kusaidia kukomesha ufujaji wa fedha za umma.

**Ikumbukwe kuwa kila mwaka mbio za Mwenge wa Uhuru zinapofanyika, kumekuwapo na kuikataa baadhi ya miradi ya maendeleo, kutokana na kwamba imetekelezwa chini ya kiwango.**

Ukweli ni kwamba, ufujaji wa fedha za umma, umekwamisha maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla, hivyo ni vyema wananchi wakashiriki kikamilifu kujua ni nini kinaendelea kwenye eneo lao.

Wananchi kuwa pembeni, inaweza kuwa ni fursa kwa wafujaji kutumia fedha za miradi kwa manufaa yao na kuitekeleza chini ya kiwango, kitendo ambacho kinaisababishia serikali hasara.

Ninadhani taarifa za ubadhirifu wa fedha za Umma ambazoi huibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katikka maeneo mbalimbali, unaweza kuchangiwa na kutoshirikishwa wananchi. Hivyo, ni vyema sasa wakielimishwa kupitia mafunzo maalum ili wanapobaini ubadhirifu wasilalamike, badala yake watoe taarifa ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria haraka iwezekanavyo.

Kimsingi hayo yakifanyika, inawezekana ripoti ya CAG isijae 'madudu' na pia Mwenge wa Uhuru hautakataa kuzindua baadhi ya miradi ya maendeleo, kwani yote itakuwa imejengwa kwa kiwango kinachotakiwa. Ikumbukwe kuwa kila mwaka mbio za Mwenge wa Uhuru zinapofanyika, kumekuwapo na kuikataa baadhi ya miradi ya maendeleo, kutokana na kwamba imetekelezwa chini ya kiwango.

Lakini kama wananchi katika maeneo husika wangekuwa wanajua umuhimu wa kufuatilia miradi yao, wangekuwa wepesi kufuatilia, kubaini na kuchukua hatua, ili kukomesha vitendo wa ubadhirifu.

Vilevile, ingekuwa ni vyema iwapo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), haitasubiri taarifa za ubadhirifu kutoka kwa CAG ndipo ifanye uchunguzi, badala ifuatulie miradi tangu mwanzo. Ubadhirifu wa fedha za umma na rushwa si kwamba si tu adui wa haki tu, bali pia inachelewesha maendeleo na vinaweza kusababisha lengo la kuifanya Tanzania iendelee kupiga hatua zaidi kiuchumi.

## HABARI KITAIFA

# Sababu wastaafu kulipwa pensheni

**Na Khalfan Said,** MBEYA

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, amesema utaratibu wa pensheni unalenga kumsaidia mtumishi wa umma atakapostaafu.

Kashimba aliyasema hayo juzi katika banda la Wizara ya Fedha alipoongoza timu ya watumishi wa mfuko huo kutembelea wanachama chini ya kampeni ya 'Banda kwa Banda' yenye lengo la kuwafikia na kuwapa elimu ya mfuko wanachama huko waliko katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo, maarufu Nanenane kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya.

Maonesho hayo yenye kaulimbiu 'Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula', yalifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango Agosti Mosi mwaka huu na kilele chake kilikuwa jana, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa mgeni rasmi.

Katika kampeni hiyo ya Banda kwa Banda, Kashimba aliyefuatana na Meneja wa PSSSF Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ramadhani Mgaya, Ofisa Uhusiano Mkuu, Abdul Njaidi na Ofisa Uhusiano Mwandamizi, Coleta Mnyamani, alisema utaratibu wa pensheni ni mfumo ambao haukujengwa kutoa fedha wakati wowote bali umejengwa kutengeneza mfuko wa pamoja wa kumwezesha mfanyakazi pale anapostaafu awe analipwa pensheni mpaka atakapofariki dunia.

"Tukumbuke kwamba huyu mtu amefanya kazi akiwa analipwa mshahara na mwajiri wake, siku akiondoka kazini anaishije? Ndipo mifuko ya pensheni ikiwamo PSSSF inaingia hapo kujibu tatizo hilo," alisema

Kashimba alisema kwa sasa umri wa kuishi umeongezeka, akitolea mfano wa mmoja wa wanachama wa PSSSF ambaye sasa anakaribia kufikisha umri wa miaka 100 na anaendelea kufaidika na pensheni.

Akizungumzia umuhimu wa hifadhi ya jamii, Kashimba alisema: "Siyo kila mstaafu ana uwezo wa kufanya biashara, hasa kwa mfumo tuliolelewa wa kuishi kwa kutegemea mshahara wa kila mwezi.

"Hivyo, pensheni ya kila mwezi inamfanya mstaafu asione tofauti ya kipato. Pensheni ya mwezi inamfanya aishi kama yuko ofisini na anaendelea kuipa huduma familia yake."

Akitoa maoni yake kuhusu huduma za PSSSF, Mkurugenzi wa Usimamizi Rasilimali Watu na Utawala Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Kennedy Nyoni, alisema BoT imekuwa na ushirikiano mzuri na PSSSF.

"PSSSF inafanya kazi vizuri na kwa kweli tumekuwa tukishirikiana kwa karibu sana." alisema Nyoni.

Mabanda waliyotembelea maofisa wa PSSSF ni pamoja na ya Wizara ya Fedha ambalo linajumuisha taasisi zote zilizo chini yake, Benki ya Azania, Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa, Chuo Kikuu ha Dar es Salaam (UDSM), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).



Fundi wa mashine za kielektroniki (EFD), Awadhi Mhavile (kulia), Ally Msesya (katikati) na Salma Ndauka (kushoto), wakiziba sura zao kukwepa kamera, walipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Kinondoni, Dar es Salaam juzi, wakikabiliwa na mashtaka saba yakiwamo ya kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 954.5. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Fundi EFD mahakamani kwa mashtaka saba

**Na Grace Gurisha**

FUNDI wa mashine za kielektroniki (EFD), Awadhi Mhavile (39) na wenzake wawili, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Kinondoni, wakikabiliwa na mashtaka saba yakiwamo ya kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 954.5.

Washtakiwa wengine ni Ally Msesya, maarufu Ally Yanga (37), mkazi wa Pugu na Salma Ndauka (38), mkazi wa Sinza ambaye ni msimamizi wa gereji. Walifikishwa juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Franco Kiswaga na kusomewa mashtaka yao.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Emmanuel Medalakini, akisaidiana na Wakili wa Serikali, Auni Chilamula, walidai washtakiwa wanatuhumiwa kwa mashtaka saba ambayo waliyatenda kati ya Mei na Julai mwaka huu ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Wakili Medalakini alidai katika shtaka la kwanza, kati ya Mei 17 na Julai 2023, maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa pamoja walitumia isivyo halali mashine za kielektroniki za EFD zilizofungwa na TRA na kutoa risiti zisizowanufaisha walipakodi wengine kudai Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh. 954,596,372 na kumpotosha kamishna wa mamlaka hiyo.

Vilevile, inadaiwa kuwa katika tarehe na mwezi huo, washtakiwa wote kwa pamoja walitumia mashine zilizofungiwa kumdanganya kamishna kutoa risiti zisizo sahihi na kuwanufaisha walipa kodi wengine kudai Sh. 954,596,372.

Medalakini alidai shtaka la tatu linamkabili Mhavile, ambaye inadaiwa Julai 8, 2023, alikutwa na mashine za kielektroniki 22 zinazodhaniwa kuwa za wizi au kuchukuliwa kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa Julai 19 mwaka huu, maeneo ya Sinza A, wilayani Kinondoni, Ndauka alikutwa na mashine 10 za EFD zidhaniwazo kuwa za wizi au kuchukuliwa kwa njia ya isiyo halali.

Katika shitaka la tano linalomkabili Mhavile, inadaiwa kuwa Julai 8 mwaka huu, maeneo ya Lumumba, jijini Dar es Salaam, alikutwa na mashine 10 za EFD na kutoa risiti za kielektroniki kinyume cha sheria.

Medalakini aliendelea kudai kuwa washtakiwa wote kwa pamoja kati ya Mei 13 na Julai mwaka huu, mkoani Dar es Salaam, waliisababishia serikali (TRA) hasara ya Sh. milioni 954.5.

Katika shtaka la saba la utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Mei 13 na Julai mwaka huu, mkoani Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa pamoja walitumia mashine za EFD kutoa risiti zisizo halali zilizotumiwa na walipakodi wengine kudai VAT ya Sh. milioni 954.5 kwa TRA wakati wakijua kwamba fedha hizo ni zao la kuisababishia serikali hasara.

Hakimu Kaswaga aliwataka washtakiwa hao kutojibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi na haijapewa kibali na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

Wakili wa Utetezi, Kesiel Kikoti, alidai kwa mujibu wa katiba washtakiwa hao kwa kuwa bado wanatuhuma, wana haki ya kupata dhamana hivyo aliiomba mahakama hiyo kuwapa dhamana wakati wakisubiri upelelezi kukamilika.


Wakili Medalakini alidai makosa wanayoshtakiwa hayana dhamana kwa mujibu wa kifungu cha 148(5)(a), hivyo maombi yao ya dhamana hayana mashiko.

Akitoa uamuzi kuhusu hoja hiyo, Hakimu Kiswaga alisema kwa mujibu wa sheria, kifungu cha 148(5)(a) kinataja makosa ambayo hayapaswi kupewa dhamana, ikiwamo utakatishaji fedha.

Alisema kwa msingi huo, washtakiwa wataendelea kukaa rumande hadi Agosti 21 mwaka huu kesi yao itakapoitwa kwa ajili ya kutajwa.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# EWURA: Acheni kuuza petroli katika vikopo

**Na Thobias Mwanakatwe,**

MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekumbusha ni marufuku kwa wananchi kuuza mafuta ya petroli na dizeli katika vikopo, ikionya kuwa ni hatari kwa mazingira na usalama wao.

Ofisa Huduma kwa Wateja wa EWURA, Francis Mhina, akizungumza jana baada ya Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda kutembelea banda la mamlaka hiyo katika Maonyesho ya Nanenane jijini hapa, alisema mafuta ni vilipuzi hatari, hivyo vinapotunzwa ndani ya nyumba vinaweza kulipuka na kuleta madhara.

Alisema EWURA kwa kutambua hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na mtindo wa kuuza wa mafuta katika vikopo, hususani vijijini, imeweka mazingira mazuri kwa watu wanaotaka kujenga vituo vya mafuta vya gharama nafuu vijijini ambavyo gharama yake ni kati ya Sh. milioni 80 hadi 85.

Mhina aliwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo ya kujenga vituo vya gharama nafuu vya kuuzia mafuta maeneo ya vijijini ili kuondokana na tabia hiyo ya kuuza mafuta katika vikopo.

Alisema EWURA imeandaa mazingira rahisi kwa watu wanaotaka kujenga vituo vya gharama nafuu vya kuuzia mafuta vijijini ambapo kibali cha ujenzi wa kituo kijijini ni Sh. 50,000 wakati mjini ni Sh. 500,000 na leseni ya kuuza mafuta kwa kijijini ni Sh. 100,000 wakati kwa mjini ni Sh. 1,000,000.

Pia alitoa tahadhari kwa wananchi kunapotokea ajali ya gari la mafuta, wasikimbilie kwenda kuchukua mafuta kwa kuwa ni hatari endapo kutatokea mlipuko.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Elimu na Huduma kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo, kuhusu matumizi ya mfumo wa kuhakiki stempu kielektroniki katika vinywaji unaosaidia watumiaji kulinda afya zao na pia kusaidia katika ukusanyaji kodi na mapato nchini unaotolewa na kampuni ya SICPA Tanzania, wakati wa maonyesho ya wakulima Nanenane viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwanafunzi wa UDSM abuni mashine ya kukausha korosho

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

MWANAFUNZI wa mwaka wa nne anayesomea Uhandisi Kilimo na Mitambo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hawa Juma, amegundua na kutengeneza mashine ya gharama nafuu ya kukausha korosho.

Hatua ya mwanafunzi huyo kutengeneza mashine hiyo inatokana na utafiti wake aliofanya kwa wakulima wa korosho mkoani Lindi na kubaini wamekuwa wakitumia njia za kienyeji kukausha korosho kwa jua kwa kuweka chini na kusababisha korosho zinazozalishwa kukosa ubora na kushindwa kumudu masoko na hatimaye kupata hasara.

Katika banda la UDSM kwenye Maonyesho ya Nanenane jijini hapa jana, Hawa alisema mashine hiyo imeshafanyiwa majaribio katika maeneo mbalimbali na kuonyesha ufanisi.

Alisema Tanzania huzalisha korosho zaidi ya tani 10,000 kwa mwaka. Asilimia 90 hupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kubanguliwa na kurudi kama korosho ambayo imekuwa ikiuzwa kwa bei kubwa huku wakulima wakipata hasara.

Alisema wapo wakulima wanaotumia njia ya kukaanga korosho au kuzichemsha, wakishamaliza wanazianika juani na kujikuta wanatumia siku nyingi kuzisubiria kukauka.

Alisema sababu hizo ndizo zilimfanya kupata wazo la kutengeneza mashine hiyo ya gharama nafuu kwa wakulima, ikiwa na uwezo wa kukausha mazao mengine zaidi na kuyafanya kuwa bora.

Alisema mashine hiyo ya kisasa mbali na kukausha, pia inasaidia kupunguza uchafu katika korosho unaotokana na upepo au vumbi.

Mhadhiri, Mtafiti na Mshauri wa Kilimo, Usalama, Chakula na Mazingira, Dk. Athuman Mahinda, alisema wamepeleka katika maonesho hayo bidhaa zilizofanyiwa utafiti na wanataaluma wakiwamo wanafunzi wa elimu ya juu na miradi sita ya wanafunzi wa shahada ya awali ambayo minne ya wanafunzi na miwili ya wafanyakazi.

# Wakulima wakoshwa mfumo uhakiki mbegu kiteknolojia

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wametoa rai kwa wakulima wenzao wa mazao mbalimbali kujisajili katika mfumo wa kuhakiki mbegu kiteknolojia wa T-Hakiki pamoja na Wakala Digital ili kuondokana na kilio cha matumizi ya mbegu feki.

T-Hakiki na Wakala digital ni mifumo ya kiteknolojia iliyobuniwa na kampuni ya Quincewood Group Limited kwa lengo la kuwasaidia wakulima kuhakiki pembejeo zao ikiwamo mbegu na kudhibiti matumizi ya mbegu feki, kuwezesha wakulima kupata pembejeo kwa wakati, kupata taarifa za Ofisa ugani katika maeneo yao na kuwasaidia wakulima kupata soko la uhakika la mazao yao.

Walitoa rai hiyo juzi waliposhiriki mafunzo ya namna ya kutumia mifumo hiyo katika Maonyesho ya Nanenane katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya.

Wakulima hao wakiwamo Innocent Michael kutoka Kasulu Kigoma na Justin Kitarima kutoka Kilolo, Iringa, walisema mbali na faida za kuhakiki mbegu wanazotumia katika mashamba yao kuwa ni halisi au feki, pia wamekuwa wakipata maelezo ya uhakika kuhusu mbegu hizo na huduma muhimu kutoka kwa maofisa ugani walioko karibu yao.

"Ni kwa kutumia simu yako tu ya mkononi, haijalishi ni simu janja au kitochi, zote ukiingiza namba *148*52# unahakiki mfuko wa mbegu ulioununa pamoja na maelezo ya kutosha ambayo kwa hakika yametusaidia sana katika shughuli zetu za kilimo," alisema Michael ambaye ni mkulima wa mahindi na kiongozi wa kikundi cha wakulima 100 kutoka Kasulu mkoani Kigoma.

Alisema kuwa baada ya kupatiwa mafunzo na kampuni ya Quincewood kuhusu mfumo wa T-Hakiki namna ya kuhakiki mbegu, sasa wanalima huku wakiwa na uhakika wa kupata mavuno bora kutokana na kutumia mbegu bora zilizohakikiwa pamoja na maelekezo sahihi kutoka kwa wataalamu wa ugani kupitia mfumo huo wa Wakala Digital.

"Tunapata maelezo ya kutosha kuanzia tarehe ya kutengenezwa kwa mbegu hizo na muda wa kuisha kwake. Kwa ujumla, tunapata maelezo ya kutosha na mkulima kuamua kufanya uchaguzi wake. Hakika T- Hakiki na hawa Wakala Digital wametusaidia sana," alipongeza.

Maelezo hayo ya Michael yanaungwa mkono na mkulima wa mahindi, nyanya na mazao mengine, Justin Kitarima ambaye alisema ni dhahiri Wakala Digital wamewapatia kitu ambacho wanakwenda kukitumia kuwaelimisha wenzao.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Quincewood Group Limited, Fatma Fernandes, alisema wamekuwa na mwendelezo wa kutoa mafunzo hayo ya namna ya kutumia mifumo ya kidijitali T-Hakiki na mfumo wa Wakala Dijital ili kuwawezesha wakulima kupiga hatua na kulima kibiashara.

"Ninampongeza sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukigeuza kilimo kuwa biashara. Pia ninampongezaWaziri wa Kilimo, Hussein Bashe kwa kuhakikisha wanawake na vijana tunaingia katika kilimo na kutambua mifumo hii ya kiteknolojia kuboresha sekta hii. Tunaona kabisa kuwa kilimo kinalipa," alisema.



# TAKUKURU yaiwezesha TRA kukusanya mil.300/-

**Na Oscar Asenga,** TANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Tanga imeiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mkoani hapa kukusanya zaidi ya Sh.milioni 300 za kodi ya zuio.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Kamanda TAKUKURU Mkoa wa Tanga, Victor Swella, wakati akitoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya Habari.

Victor alisema katika kutekeleza jukumu hilo kwa kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka 2023 walifanya uchambuzi wa mifumo kuhusiana na ukusanyaji wa kodi ya zuio.

Aidha, alisema uchambuzi huo ulihusisha pia ukusanyaji wa kodi ya zuio na uchukuaji wa risiti za mfumo wa kielekroniki (EFD), katika malipo yanayohusiana na manunuzi mbalimbali ya bidhaa na huduma katika halmashauri zote za mkoa huo.

Hata hivyo, alisema malengo ya uchambuzi yalikuwa ni kubaini mianya ya rushwa kwenye utoaji wa risiti za EFD kwa halmashauri na ununuzi wa huduma au vifaa na ukataji wa kodi ya zuio kwa huduma au bidhaa zinazonunuliwa na halmashauri hizo.

Alisema baada ya mchakato huo, walishauri namna bora ya kuboresha na kusimamia matumizi ya risiti za EFD na ukataji kodi ya zuio katika manunuzi ya bidhaa na huduma.

Alisema yaliyobainika ni kuwa manunuzi ya huduma na bidhaa hayakuwa na risiti za EFD na baadhi yao manunuzi ya huduma na bidhaa kutokukatwa kodi ya zuio na yaliyokatiwa fedha husika hazikuwasilishwa TRA kutokana na taasisi zinazofanya manunuzi kutosajiliwa katika mfumo wa uwasilishaji kodi ya zuio.

# TBS yawatembelea wajasiriamali kwenye maonyesho Nanenane

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewatembelea wajasiriamali wanaoshiriki Maonesho ya Wakulima Nanenane yanayofanyika katika viwanja vya Themi-Njiro jijini Arusha ili kujua changamoto zao sambamba na kuwapa elimu ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Msisitizo wa TBS kuwahimiza wajasiriamali hao kujitokeza kuthibitisha ubora wa bidhaa zao unaotokana na huduma hiyo kuwa inatolewa bure kwao, kwa kuwa Serikali inatenga kati ya Sh. milioni 150 hadi 200 kila mwaka kwa ajili ya kuwahudumia.

**TBS ipo kwenye maonyesho hayo tangu Agosti 1 yalipoanza hasa kwa kuzingatia kwamba shirika hilo ni wadau wakubwa.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye maonyesho hayo, Meneja Uhusiano na Masoko wa TBS, Gladness Kaseka, alisema hadi sasa zaidi ya wajasiriamali wadogo 600 kutoka mikoa mbalimbali wamepata leseni chini ya mpango huo bure.

Alisema TBS ipo kwenye maonyesho hayo tangu Agosti 1 yalipoanza hasa kwa kuzingatia kwamba shirika hilo ni wadau wakubwa.

"Kwa hiyo tupo kwenye viwanja hivi kwa ajili ya kusikiliza changamoto, kuzitatua na kutoa elimu na kuwapa msaada wadau wetu kuhusiana na huduma mbalimbali za shirika," alisema Kaseka.

Kwa mujibu wa Kaseka, miongoni mwa huduma hizo ni pamoja na usajili wa bidhaa na majengo ya chakula na vipodozi, leseni ya kutumia alama ya ubora na msaada wa kitaalamu kwa wanaosafirisha bidhaa nje ya nchi pamoja na umuhimu wa kusoma taarifa za kwenye vifungashio hususani kujua muda wa mwisho wa matumizi wa bidhaa husika.

Kaseka alitoa wito kwa wateja na wananchi kutumia fursa hiyo kwa kutembelea banda la TBS lililopo ndani ya viwanja hivyo na watakaoshindwa wasisite kuwasiliana na TBS kupitia kituo cha huduma kwa wateja.



Ofisa Lishe wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Emmanuela Lawrence (kulia), akitoa elimu ya unyonyeshaji kwa wakinamama na kugawa uji wenye lishe bora kwa watoto wadogo katika maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji duniani katika zahanati ya kata ya Tongwe, wilayani juzi. Kushoto Katibu wa Afya wa wilaya hiyo, Merenia Faustine. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# SGA yaibuka kinara kampuni bora ya ulinzi Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA Security imetangazwa mshindi wa jumla kati ya kampuni za ulinzi Afrika katika tuzo za kampuni bora Afrika zilizofanyika mwishoni mwa wiki.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya SGA Tanzania, Eric Sambu alisema kampuni hiyo imepitia wakati mgumu baada ya ongezeko ghafla la kima cha chini cha mshahara kwa asilimia 48, jambo ambalo lilifanya wateja wengi washindwe kumudu gharama za ulinzi lakini kwa sasa hali imetengamaa.

Alisema kampuni hiyo inajiandaa kuadhimisha miaka 40 ya kutoa huduma nchini Tanzania na kusema kuwa SGA ndiyo ilikuwa kampuni ya kwanza ya ulinzi ya binafsi kusajiliwa Tanzania huku ikijulikana kama Group 4 Security (T) Ltd mwaka wa 1983.

Alisema SGA imeleta mabadiliko makubwa katika sekta ya ulinzi Tanzania tangu muda huo na imeajiri Watanzania zaidi ya 5,000 ambao ni sehemu ya wafanyakazi 18,000.

Aidha, aliwapongeza askari wa kampuni hiyo kwa ubora wao ambao unaifanya SGA iwe juu ya kampuni zingine.

"Kuna ziadi ya kampuni 2,000 ya ulinzi nchini Tanzania lakini kinachotutofautisha ni namna tunavyotoa huduma zetu. Tunawapa kipaumbele wafanyakazi wetu ili waendelee kufanya kazi kwa weledi na hata kuzidi matarajio ya wateja wetu," alisema.

Sambu alisema wanafurahia ushirikiano kati ya kampuni zake na mashirika ya serikali hasa Jeshi la Polisi ambalo wanashirikiana nalo katika mafunzo, kuchuja maaskari wakati wa kuajiri, uchunguzi na katika kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu.

Hivyo, alitoa wito kwa kampuni zingine za ulinzi kuiga mfano huu kwa kuwajali wafanyakazi wao ikiwemo kuwalipa vizuri kama njia ya kuwapa motisha ya kufanya kazi kwa bidii. "

Alisema wataendelea kuwekeza katika watu, teknolojia na ubunifu ili kuwapa wateja huduma bora zaidi.

Naye Meneja Masoko wa SGA, Faustina Shoo alisema wamefarajika kupokea tuzo hiyo hasa baada ya kupitia kipindi kigumu kilichosababishwa na janga kubwa la ugonjwa wa virusi vya corona.

# Idadi ya watalii wanaoshuka KIA yazidi kuongezeka

**Na Daniel Sabuni,** KILIMANJARO

IDADI ya wageni wanaoshuka kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), imeongezeka kutoka 300 hadi kufikia 2000.

Ongezeko hilo limechangiwa na Filamu ya The Royal Tour iliyoigizwa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uendashaji wa Kiwanja cha Ndege cha KIA (KADCO), Christina Mwakatobe, wakati wa hafla ya kuwapokea watalii 54 kutoka nchini ugiriki waliofika kwa mara ya kwanza.

Alisema idadi ya watalii imeendelea kuongezeka kwa kasi kutoka watalii 780,000 mwaka 2019 kabla ya UVIKO 19 hadi 927,000 mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia 42.

Alisema: "Sasa hivi uwanja huu tunashuhudia makundi makubwa ya watalii, kwa siku moja hadi watalii 2,000 jambo linaloonyesha matokeo chanya ya kutangaza vyema utalii nje kutokana na Filamu ya The Royal Tour".

Aidha alisema kuna mashirika ya ndege yameongeza idadi ya miruko sambamba na uwapo wa ndege za watalii binafsi wanaokuja kutembelea vivutio.

Wakala wa utalii ambaye ameleta watalii hao kutoka Ugiriki, Manasse Kidman, alisema watalii hao watakaa kwa muda wa siku tatu na wanatarajia kwenda maeneo mbalimbali ikiwamo Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mmoja wa watalii hao, Christos Gianakopoloulos, alisema matarajio yake ni kuona wanyama wakuu watano ambao aliambiwa Tanzania ni rahisi kuwaona kuliko nchi nyingine yeyote.



# Vijana, wanawake wajitosa kulima, kufuga kisasa

**Na Aneth Ntungo,** SAUT

VIJANA na wanawake kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa Magharibi wameonesha kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha wanalima na kufuga kisasa lengo likiwa ni kujiinua kiuchumi na kuacha kutegemea kuajiriwa sambamba na kukuza sekta ya kilimo.

Hii imejidhihirisha katika maonesho ya kilimo, mifugo na uvuvi (Nanenane) yaliyomalizika jana mkoani Mwanza katika viwanja vya Nyamhongolo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti vijana na wanawake hao wameeleza kuwa kilichowasukuma kushiriki katika maonesho ya mwaka huu ni jinsi serikali ilivyowapa kipaumbele kwa kauli mbiu isemayo 'Vijana na wanawake ni msingi imara wa mifumo endelevu ya chakula'.

Kijana mfugaji wa kuku, Julius Sadala alieleza kuwa kwa sasa kama vijana wameshtuka na kuona kuwa kuendelea kusubiri ajira ni sawa na kuendelea kujichelewesha katika mafanikio hivyo kutakiwa kufanya kazi zenye tija na faida kwao.

**Kwa kupitia maonesho hayo amekuwa akishiriki pia kutoa elimu ya ufugaji wa kuku wa mayai na nyama kwa vijana na watu wengine lengo likiwa ni kuwasaidia kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli za ufugaji.**

"Maonesho haya yamekuwa msaada mkubwa kwangu katika kuzitangaza kazi zangu za ufugaji na kila uchwao nimekuwa nikiongeza wateja na ufanisi wa kazi kutokana na maonesho ya namna hii kwani wapo wataalam mbalimbali wenye ujuzi zaidi ya ule nilionao," alieleza Sadala.

Kadhalika, alisema kuwa kupitia maonesho hayo amekuwa akishiriki pia kutoa elimu ya ufugaji wa kuku wa mayai na nyama kwa vijana na watu wengine lengo likiwa ni kuwasaidia kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli za ufugaji.

Leticia Ntubija mkazi wa Wilaya ya Kwimba na kiongozi wa kikundi cha wakulima wa mpunga aliieleza Nipashe kuwa kikundi chao wamekuwa wakijishughulisha na kulima mpunga, kukoboa na kuuza mchele na kwa kufanya hivo wamekuwa wakijipatia kipato na kuendesha maisha yao.

Aidha, alisema kuwa kikundi chao kinahusisha wanawake na vijana kwa wingi kwasababu vijana na wanawake wanafanya kazi kubwa katika kuinua uchumi wa taifa na wamepewa kipaumbele ili kujitokeza katika shughuli za uzalishaji mashambani, viwandani na hata sokoni.

Dk. Nkwabi Joel mtafiti wa mbegu za mazao ya biashara na chakula kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Nchini TARI Ukirigulu akizungumza na Nipashe aliwataka vijana na wanawake kujikita katika kilimo cha mazao yanayoimiri ukame ili kuepuka na hasara.

Alitaja mazao hayo kuwa ni pamoja na maharage ya Jeska, mihogo pamoja na mtama mweupe aina ya tariso 1 wenye uwezo wa kuzalisha tani nne katika hekari moja unaovumilia magonjwa pamoja na ukame.

Maonesho hayo yalifungwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makala huku akiwataka vijana kuendelea kuchangamkia fursa za mikopo ambayo itawasaidia katika kuinua uchumi wao kupitia kilimo na ufugaji.




Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima (wa tatu kulia), akigawa vyandarua vyenye dawa kwa baadhi ya wananchi waliohudhuria uzinduzi rasmi wa kampeni ya ugawaji wa vyandarua hivyo, kwenye kaya za Mikoa ya Tabora na Kagera katika viwanja vya Mashujaa, Mjini Bukoba juzi. Kulia ni Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel na (wa pili kulia) ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kagera, Nazir Karamagi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji madini waomba msaada vifaa

**Na Timothy Itembe,** MARA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu kutoka Kerende Halmashauri ya Tarime wameiomba serikali kuwatengenezea mazingira rafiki ya kupata vifaa saidizi vya uchimbaji madini ambavyo watavinunua kwa gharama nafuu ili kufanya uchimbaji wenye tija.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti na kueleza kuwa wamekuwa wakifanya kazi hiyo kwa mazoea hali ambayo imekuwa ikisababisha uzalishaji wao kuwa chini tofauti na inavyotegemewa.

Mmoja wa wachimbaji hao kutoka mgodi wa wachimbaji wazawa, Kasara Nyamohanga, alisema kuwa kuna haja serikali kuwatengenezea mazingira rafiki ya kulipa kodi huku wakijua kuwa wanatumia gharama ya mitaji yao kuchimba mashimo.

Maisa aliongeza kuwa mawe ya dhahabu yanatolewa kwa utaratibu uliokubalika na wafanyakazi wa mashimo wanapata mishahara kwa utaratibu uliokubaliwa, serikali itoze kodi baada ya kuuza na kutoa gharama za uwendeshaji za mmiliki wa shimo.

Elizabeth Waitara, mfanyabiashara katika eneo hilo alisema wanatumia fursa hiyo kufanya biashara ndogo ili kujipatia fedha za mahitaji ya kifamilia ikiwemo kusomesha watoto.

Aidha, aliomba mazingira ya kufanyia shughuli hiyo yaboreshwe pamoja na kuchukuliwa tahadhari za kiusalama kabla ya hatari kutokea.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kerende, Mniko Magabe, alieleza kuwa idadi kubwa ya wachimbaji wadogo na wazawa katika eneo hilo wamekuwa wakitumia vifaa duni vilivyopitwa na wakati hali ambayo imekuwa ikididimiza shughuli zao za uchimbaji madini.

Alisema kutokana na wachimbaji hao kuwa chachu kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya machimbo ni vyema serikali ikawasaidia kupata vifaa vya kisasa kwa gharama nafuu ili waweze kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa madini hayo.

Kuhusu utoro wa watoto kwa eneo hilo, aliwataka watoto kuacha tabia ya kwenda mgodini kuokota mawe yanayodhaniwa kuwa na dhahabu.

# Hospitali yaiangukia jamii kujitolea kuchangia damu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HOSPITALI ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imeomba jamii kuwa mstari wa mbele katika kuchangia damu salama ili kuwasaidia kuondokana na adha ya ukosefu wa damu ili kukabiliana na vifo vya wajawazito, watoto na majeruhi wa ajali.

Hospitali hiyo kwa siku inatumia uniti 10 hadi 15 kulingana na uhitaji wa wagonjwa, huku kwa mwezi mmoja wanatumia uniti 300 hadi 450 hali ambayo inawalazimu kupita katika shule za msingi, sekondari na kwenye mikusanyiko mbalimbali ili kupata damu.

Mratibu wa Damu Salama, Noel Malaki aliyabainisha hayo juzi wakati wa maadhimisho ya mwaka mpya wa kislamu wa 1,445 uliombatana na uchangiaji wa damu salama kwa vijana 218 wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Dini Kislamu(JUVIKIBA) yaliyofanyika katika Msikiti wa Ijumaa na kuhudhuriwa na viongozi kutoka mikoa ya Tabora na Mwanza.

Alisema, uhitaji wa damu katika hospitali ya Manispaa ya Kahama ni mkubwa, kwa sababu imekuwa ikitoa huduma kwa wananchi kutoka mikoa mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Msalala, Ushetu, Shinyanga vijijini, Wilaya za mikoa ya Tabora, Kigoma na Geita.

Shekhe wa Wilaya ya Kahama, Omari Damka, aliwapongeza vijana kwa kusherehekea mwaka mpya wa kisalamu wa 1,445 kwa kuchangia damu hospitalini, itakayosaidia kuokoa maisha ya wajawazito, watoto na waliopata ajali na kuwataka kuendelea kuhimizana kuwa na utaratibu wa kufanya hivyo mara kwa mara.

Mwenyekiti wa JUVIKIBA, Hassani Haruna alisema, lengo la kuanzisha umoja huo ni kuwa kitu kimoja na kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo kuchangia damu, kupinga vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya, ndoa na mapenzi ya jinsia moja na ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto, wanawake na wazee wanaoishi pembezoni.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, Azan Saidi aliwataka vijana hao kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali ili waweze kupata fursa ya kupewa mitaji ya kufanya biashara.

**Uhitaji wa damu katika hospitali ya Manispaa ni mkubwa, kwa sababu imekuwa ikitoa huduma kwa wananchi kutoka Halmashauri ya Msalala, Ushetu, Shinyanga vijijini, Wilaya za mikoa ya Tabora, Kigoma na Geita.**



Ukurasa 12

**JUHUDI KUFIKIA 50/50**
**Kifahamu kinachokwamisha kinamama kuchukua uongozi**


Ukurasa 13

**UTAWALA BORA NA JINSIA VISIWANI...**
Watafiti wabaini kinamama kwenye habari sauti yao bado iko 'uvunguni'

siasa
JUMATANO AGOSTI 9, 2023
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU


Ukurasa 14

**NAJLA BOUDEN**
**Waziri Mkuu profesa, aliyetumbuliwa kukwepa mipango hatarishi ya IMF**

# Tathimini ya kina Mkataba wa Bandari unavyokaribisha ahueni

**Na Nimi Mweta**

MOJA ya maswali ambayo yanajitokeza katika mjadala wa makubaliano ya uendeshaji Bandari ya Dar es Salaam ambako Tanzania itafanya kazi na kampuni ya DP World ya Dubai, ni iwapo kuna aina tofauti za mikataba na ufanisi unaofanana.

Sababu ya kufuatilia swali hilo ni kuwa uendeshaji wa chochote kile katika karne hii ya teknolojia ya mawasiliano ni mifumo inayotumika, hivyo kushirikiana na DP World hasa ni kuwa na teknolojia yao, na kuwapa nafasi ya kisheria ya kuisimamia na kuitumia ipasavyo.

Ni tofauti na kukodisha bandari na wananchi wanapofika eneo hilo wawe wageni unakuwa mwanzo wa kukwazika.

Ukijaribu kufuatilia kilichomo katika majarida ya kitaalamu kuhusu suala hilo na siyo hoja za wachangiaji kwenye mitandao ya kijamii au majukwaa ya siasa, unakuta ipo mikataba ya aina tofauti inayotumika katika eneo hilo.

Kuna utafiti wa mwaka 2012 unaotajwa chini ya fani ya 'uchumi wa bandari,' unaolenga umiliki na uendeshaji wa kitengo cha makontena kilichokodishwa. Ina maana mikataba hiyo si ya kukodisha bandari yote. Ni eneo mahsusi la bandari ambalo uendeshwaji wake na mwenye mkataba hubadili sura ya kazi inayofanyika na kuongeza ufanisi hasa kwa washindani nje.

Utafiti unasema moja kati ya bandari nne kote duniani imetoa eneo la kutia nanga meli na kushusha shehena kwa zabuni za kiushindanishi, ila si zote. Maeneo mengine kuchagua kampuni ya uendeshaji inafanana na 'shindano la urembo' ambako maombi ya kampuni zenye shauku ya kuendesha yanapokelewa bila kuyaanika hadharani na inayofaa huteuliwa.


Kitengo cha Makontena cha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. **PICHA: MTANDAO**

Katika jambo hilo peke yake unaweza kuvuna ubishi mwingi, kwani watetezi wa zabuni wanawaaminisha watu kuwa bila hivyo atateuliwa mwendeshaji kutokana na maslahi binafsi, kukaribisha tenda hakuzuii maslahi binafsi, ila ni mamlaka husika zitakazoendesha ushindani, na serikali ichukue itakachopewa.

Aidha, utafiti unasema nusu ya bandari ambazo sehemu zake zimekodishwa zina mfumo huo wa makubaliano, ambako mamlaka za nchi zinaangalia uendeshaji maeneo tofauti na kufikia uamuzi ni kampuni gani inafaa. Ubishi unaoletwa kwa suala hilo huwa ni dharau kwa mamlaka za kisiasa, na kutaka masuala yote yafanyike kitaaluma, wakati hapo pia kuna maslahi binafsi yanayotarajiwa, ya kutoingiliwa na wasimamizi wizarani. Hisia hiyo ina nguvu hapa nchini hasa kutokana na uchanga wa sekta binafsi, licha ya kuwa hali hiyo imepungua ukilinganisha na miaka ya 1990, wakurugenzi wakipinga kwa nguvu kuingiliwa.

Kuna aina nyingine ambako mwendeshaji anajenga eneo mahsusi la bandari na kuwa huru kuongeza maeneo ya kutia nanga na kupakua shehena ila mikataba hiyo inakuwa na vipengele au kufanyiwa marekebisho, kuruhusu waendeshaji wengine wakodishiwe nafasi hizo au wajenge za ziada kulingana na mahitaji.

Kipengele hicho kwa suala la DP World kinahusu bandari ya Bagamoyo, wajenge vituo vya kupokea meli, waendeshe na kulipa kodi serikalini, au wakodishiwe vituo vilivyopo bandari ya Dar es Salaam. Utatuzi wake unaweza kuwa ni ujenzi wa bandari hiyo mpya na waendeshaji kuhamishia shughuli huko zaidi, ndani ya miaka 10.

Aina nyingine ya mkataba ambao huenda ndiyo inayopendwa zaidi na wapinzani wa mkataba uliopo ni ukodishaji unaolengwa kati ya wapakuaji mizigo ndiyo hao pia wapakiaji melini na wasafirishaji mizigo wakubwa wenye meli.

Unakuwa na vituo vya Maersk, MSL, PO, CMA CGM, Lloyd, COSCO (China Ocean Shipping Company) kila mmoja asimamie temino yake halafu Mamlaka ya Bandari inakuwa msimamizi wa jumla au mwangalizi wa sheria na maslahi ya nchi.

Tatizo hapo ni kama uliwahi kuwapo ushawishi wa aina hiyo, kwani utafiti unaonyesha kuwa ukodishaji huo upo zaidi pwani ya Bahari ya Pacific, yaani ukanda wa magharibi wa Marekani halafu Japan kwa jumla, na uendeshaji wa maeneo hayo mawili unafanana.

Ni kutokana na wingi wa bidhaa kati yao, ambayo ina maana kuwa China ingepata bandari au vituo maridhawa pia, kama kusingekuwa na ushindani haramu kati ya Marekani na China, unaodaowa ni wa kutumia biashara kuandaa vita.

Unaweza kusema kuwa mkataba wa DP World hapa nchini unafanana na mojawapo kati ya vituo hivyo, kwani bidhaa kwa sehemu kubwa zinatoka Dubai na China. Endapo DP World imejikita katika bandari muhimu za China na hata India kwa baadhi ya mizigo, bandari ya Dar es Salaam inakuwa kama kituo kingine cha mtandao huo.

Kimsingi mkataba uliopo unalenga faida hizo, yaani kutumia mtandao wa DP World kuharakisha kuagiza, kuleta au kupeleka mizigo eneo husika, badala ya mikono mingi kushika shehena hizo, kwa tija hafifu. Ndipo un-

INAENDELEA UK. 14

JUHUDI KUFIKIA 50/50

# Kifahamu kinachokwamisha kinamama kuchukua uongozi

## •Wapikwa kushiriki uchaguzi serikali za mitaa 2024



Scola Makwaiya, akiwanoa kinamama kwenye darasa la uongozi.

**Na Sabato Kasika**

WANAWAKE wako tayari kwa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka 2024? Ushiriki wao ni jambo linalohimizwa kila wakati ili kufungua ukurasa mpana wa kuwa na Tanzania yenye uwiano kiuongozi unashabihiana wa 50/50.

Ili kuongeza idadi yao katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wenye mafanikio, kina mama ni lazima wapewe nyenzo na mbinu ili kuwa viongozi na kutimiza azma ya kile walichokuwa wanakitafuta kwa muda mrefu.

Wakati uchaguzi wa serikali za mitaa ulifanyika Novemba 2019, ni wazi mwingine hauko mbali na wadau wa usawa wa kijinsia, wameanza kutoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake kuwaandaa kushiriki uchaguzi huo.

Ni mafunzo ya uongozi yanayotolewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP). Akiwapika kinamama wa kata ya Mabwepande - Dar es Salaam, Scola Makwaiya, wa mtandao huo, anataja sababu zinazofanya wanawake wabaki nyuma kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi ya chini kuwa ni pamoja na mtindo wa baadhi yao kujiona kama hawahusiki katika masuala la uongozi.

Anakumbusha kuwa hicho, ndicho kinachelewesha taifa kufikia uongozi na uwakilishi wa uwiano wa asilimia 50 kwa 50 au ambao wamekuwa wakiutafuta kwa muda mrefu.

Anaongeza: "Lakini wanawake hatuko tayari kufuatilia taarifa mbalimbali katika maeneo yetu ili kama kuna fedha za miradi ya maendeleo zimeletwa, tujue ni kiasi gani na zinatumikaje."

Aidha, anasema kwenye masuala ya uongozi na pia ufuatiliaji miradi ya maendeleo hayana jinsi, bali wanawake na wanaume wanatakiwa kushiriki kwa ajili ya maendeleo ya maeneo yao na taifa kwa ujumla.

"Matokeo ya sensa iliyopita, yanaonyesha kuwa idadi ya wanawake ni asilimia 51 zaidi ya wanaume, hivyo tuutumie uwingi wetu katika uchaguzi wa serikali za mitaa ili tuchague wanawake wengi katika uongozi," anasema.

Halikadhalika, anawaambia wanawake kuwa ni muhimu wajitokeze kwa wingi zaidi kwenye uchaguzi wa mwaka 2024 na kwamba TGNP na wadau wengine wanaendelea kutoa mafunzo hayo sehemu mbalimbali nchini ili kuwajengea uwezo wa kiuongozi kuanzia ngazi ya chini ili waweze kushiriki kwenye chaguzi za serikali za mitaa 2024 na mkuu wa 2025.

"Malengo mahsusi ni kuongeza uelewa na umuhimu wa kushiriki katika uongozi ngazi ya jamii, kubadili mtazamo hasi kuhusu wanawake na uongozi, kwa kuangalia masuala ya kiuchumi, kiutamaduni na ushiriki wenu katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu," anasema Scola.

**MAELEWANO KIFAMILIA**

Scola anasema pamoja na mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo ili wawanie uongozi, anatoa angalizo kwamba yasiwe chanzo cha kuvunja ndoa zao, bali kila mmoja wao aangalie kama mwenza wake hamzuii.

"Sitaki TGNP ichukuliwe kama ndio chanzo cha kuvunja ndoa za watu, hivyo washawishini wanawake zenu kwa kuwaeleza umuhimu wa uongozi kwa wanaume na wanawake ili wawaelewe kwanza," anasema.

Anafafanua kuwa wapo baadhi ya wanaume hawataki kusikia wake zao wanaingia kwenye siasa kuwania uongozi, kwani wanaamini kuwa huo ni uhuni, kitendo ambacho kinakwamisha wanawake kupiga hatua akisema waume wa aina hiyo ni kuwaelimisha taratibu ili hatimaye waelewe na kuwa tayari kuwaruhusu wake zao kujitokeza na kwamba mume akikataa, mwanamke asilazimishe.

"Lakini ninaamini kuwa wanaume wengi ni waelewa watawaruhusu tu, ila mkazo wangu ni kwamba, mkienda kinyume na hapo, lawama zinaweza kuelekezwa kwa TGNP na kumbe siyo lengo letu," anasema.



Latifa Daud, akichangia hoja. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Anakumbushia kuwa wanawake wasijiweke pembeni katika suala uongozi, huku akikazia kuwa iwapo hawataruhusiwa na waume zao, waepuke kulazimisha badala yale wawaunge mkono wale ambao watakuwa huru kuwania, ili kuongeza idadi yao.

**HOFU YA TALAKA**

Hofu ya talaka inaibuliwa na Latifa Daud, mmoja washiriki wa mafunzo hayo, anayesema sababu kubwa ya wanawake kutoshiriki katika uongozi, ni kuhofia kuachwa na waume zao na hivyo kujikuta wakiwa ni watazamaji zaidi.

"Ikumbukwe kuwa mara nyingi wanaume ndio wanaomiliki mali, sasa mwanamke unataka kuwania uongozi, ambao ukweli ni kwamba lazima uwe na fedha, inakuwa ni vigumu kuchukua fedha hizo," anasema Latifa.

Latifa anafafanua kuwa mwanamke akilazimisha kuchukua fedha za mume kwenda kwenye mchakato wa uongozi, anaweza kujikuta akiachwa na hivyo kubaki akitangatanga na yote hayo yanatokana na mila, desturi na mtazamo finyu kuhusu wanawake na uongozi, kwa kuwa tangu zamani imezoeleka kuwa viongozi ni wanaume tu kuanzia kwenye familia.

"Wanawake tunapata nafasi nyingi za uongozi katika vikundi vya vikoba kwenye maeneo yetu ambako waume zetu wanaweza kuturuhusu, lakini zaidi hapo tunachukuliwa kama tunakwenda kufanya uhuni," anasema.

Hamida Nyoni anasema, uongozi sio jambo la kukimbilia, bali ni kujipanga vizuri, kwa maelezo kwamba wanawake wanaweza kuelimishwa wakaenda kuwania na kujikuta wakianguka."Jambo la kuzingatia, ni lazima mgombea ajue jamii iliyomzunguka inamkubali kiasi gani, siyo kuomba mume pesa za kampeni lakini mwishowe zikapotea bila kupata nafasi," anasema Hamida.

Aidha, anaongeza kuwa mafunzo yanayotolewa ni ya muhimu na pia ni vyema wanawake wakajipima kulingana na maeneo wanayotoka kuwa wanakubalikaje kwa jamii yao badala kujitosa tu.

Anaungwa mkono na Mwajuma Kikumbi, anayesisitiza kuwa wanawake hawana budi kujaribu, kwa maelezo kwamba wapo wengine wanaoombwa na jamii inayowazunguka kuwa wawanie uongozi lakini wanakataa.

"Ukiona jamii inayokuzunguka inakushawishi uwanie uongozi, maana yake ni kwamba imeona kitu kwako, usikate, lakini bahati mbaya wanawake wengi huwa tunakataa," anasema Mwajuma.

Aidha, anasema ni kitendo hicho cha kukataa kinachangia kuwafanya watu wakate tamaa na kuona haina haja kuchagua mwanamke kuwa kiongozi, hali ambayo inachangia kuwafanya wanawake kubaki nyuma.

"Mafunzo haya ya TGNP yatuamshe na kutufanya tuondoe woga na kutojiamini ili tuangalie jinsi jamii inavyotupenda na kutamani tuiongoze. Tukiacha woga na kutojiamini tutaweza," anasema.

Mwanajuma anasema hakuna aliyezaliwa kuwa kiongozi, bali watu wote wanawake kwa wanaume wanajifunza na kwamba kupitia mafunzo hayo, wanaenda kujiandaa kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa.



Katika picha ya pamoja, wadau wa habari na mwongozo wa sera ya jinsia ulioandaliwa na TAMWA. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

ULIVYO UTAWALA BORA NA JINSIA VISIWANI…

# Watafiti wabaini kinamama kwenye habari sauti yao bado iko 'uvunguni'

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JITIHADA za kufikia usawa wa kijinsia katika nyanja zote muhimu kuanzia uchumi, uongozi na pamoja na masuala ya kijamii haziwezi kufanikiwa bila uwapo wa vyombo vya habari.

Tasnia ya habari inatajwa kuwa ni mdau muhimu wa kuimarisha usawa wa kijinsia na ili kufikia hatma hiyo inahitajika sheria, sera na mikakati ya utekelezaji ili kuiwezesha kutoa mchango wake katika safari ya kufikisha Tanzania kwenye usawa wa kijinsia.

Ili kufika katika bandari salama kijinsia, Tanzania imesaini mikataba mbalimbali ukiwamo wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (CEDAW) wa 1979, itifaki ya Afrika na Maputo 2003 na wa Jumuiya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) wa mwaka 2008.

Hivi karibuni Chama cha Wanahabari Wanawake -TAMWA, Zanzibar, kimezindua sera ya jinsia kwa vyombo vya habari, itakayoelekeza watendaji wa tasnia hiyo kuzingatia mahitaji ya jinsia ili kufikia malengo ya taifa na dunia ya usawa kijinsia.

Dk. Mzuri Issa ni Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, anayezungumzia ujio wa sera hiyo, akisema utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaeleza kuwa, ni nadra wanawake kuonekana kama vyanzo vya habari.

Ikimaanisha kuwa wazungumzaji na watoa taarifa iwe kwenye redio, gazeti, runinga na mitandaoni wasemaji ni wanaume zaidi.

Anasema wako chini ya asilimia 30 kwa mujibu wa utafiti huo wa mwaka 2022 na kwamba TAMWA imefanya uchambuzi na kubaini kuwa vyombo vya habari vimewatumia wanawake kama vyanzo vya habari kwa asilimia 27 huko Zanzibar.

Aidha, anasema kuna ushahidi, baadhi ya watu katika tasnia ya habari wanajihusisha na rushwa za ngono ambayo huwaathiri zaidi wanawake vijana na pia kusababisha uwakilishi mdogo katika sekta hiyo.

Mzuri anasema idadi yao ni ndogo kwenye vyombo vya habari na vya maamuzi, wamiliki na wahariri.

"Hivyo vyombo vya habari kioo cha jamii kinapaswa kusimama imara kutekeleza masuala ya kijinsia ili kufikia wanawake na wanaume kufaidika katika kupata usawa na haki kwenye fursa zote," anasema na kuongeza:

"Vinahitaji muongozo ili kuweka mikakati ya kutatua changamoto zake za ndani lakini pia za wanawake katika jamii.

Anatoa mfano kwenye uongozi, tafiti zinaonesha kwamba wanawake kiuongozi ni chini ya asilimia 30 barani Afrika ukiacha mataifa ya mfano kama Rwanda ambayo yamefikia asilimia 50 kwa 50.

Aidha, Dk. Mzuri anasema tafiti zinaonyesha habari za wanawake hazipati nafasi au umuhimu mkubwa katika vyombo vya habari kutokana na mifumo dume na ukweli kuwa wanawake kwa miaka mingi wameachwa nyuma.

### UJIO WA SERA

Akizungumzia madhumuni ya sera ya jinsia anasema, ni kusaidia vyombo vya habari kuimarisha hali za wanawake katika tasnia ya habari yenyewe na jamii, kuazisha sera ya habari ikiwamo vituo au dawati la jinsia kuhakikisha utekelezaji wake.

Mzuri anawataka wadau wa maendeleo ya jinsia kutumia muongozo huo wa sera ya jinsia ulioandaliwa kwa ajili ya vyombo vya habari, akizilenga taasisi za elimu ya juu vyuo vikuu, vya kati, za serikali kuu, mitaa na za binafsi, wanaharakati na wanafunzi kuutumia ili kuweza kufanikisha kufikia usawa wa kijinsia.

Anaongeza kuwa sera ya kijinsia itatambua kanuni mbalimbali zitakazoundwa na chombo cha habari ambazo zitalipa mamlaka dawati la jinsia ya kusikiliza na kupokea taarifa mbalimbali za unyanyasaji wa kingono, kijinsia, kielimu au viashiria vitakavyokuweko sehemu za kazi ili kuchukua hatua za kinidhamu.

"Ni lazima tukubali kwamba, kazi bila ya unyanyasaji wa kijinsia inawezekana, hivyo ni lazima kuwepo kwa fursa sawa ambazo zitaepuka ukatili wa kijinsia miongoni mwetu,"anasema.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar Suleiman Abdallah, anasema ni muhimu kwa vyombo vya habari kufuata na kutumia muongozo huo wa sera ya jinsia ili kuweka usawa maeneo ya kazi, lakini pia kuondoa changamoto zinazowakabili wanawake.

Anasema ipo haja ya kuwa na maudhui kamili kuhusu athari za vyombo vya habari katika kutekeleza sera ya jinsia, akisisitiza haja kwa taasisi za habari kuwashirikisha wanawake kwenye nafasi za uongozi.

Anaongeza kuwa unapomwandaa mapema mwanamke kwenye nafasi za uongozi unamrahisishia kukabiliana na changamoto za kufikia ngazi za juu kiuongozi.

"Tuwape nafasi za uongozi waandishi wa habari wanawake katika vyombo vyetu ili kuongeza idadi ya viongozi wanawake,"anasema Abdallah.

### KUEPUSHA UMBUMBUMBU

Mwenyekiti wa Mtandao wa Kijinsia (ZGC) Asha Aboud, anaungana na juhudi za TAMWA kutayarisha na kuzindua muongozo wa sera ya kijinsia na kuwataka wakuu wa vyuo vikuu kuwa na sera hiyo pamoja na dawati la kijinsia ili kuepusha unyanyasaji wa aina yoyote ikiwamo rushwa ya ngono ambayo moja ya athari zake ni taifa kuwa na wasomi wasio na sifa au mbumbumbu wenye shahada.

Mhadhiri Imane Duwe wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), anasema kuna changamoto nyingi katika vyombo vya habari ambazo wanakumbana nazo wanawake, ikiwemo udhalilishwaji kijinsia.

"Wanakumbana na changamoto nyingi za udhalilishaji na baadhi ya vyanzo vya habari hasa wenye mamlaka serikalini huwatumia vibaya, ni vyema kuwa jasiri na kuyafichua maovu wanayofanyiwa," anasema Imane.

Anasema sera hiyo itaonyesha hali ya usawa baina ya jinsia ya kike na ya kiume katika hali zote za uchapishaji wa habari, utangazaji na urushwaji wa vipindi na wahusika ambao ni wanahabari wenyewe.

Anawataka wahariri kuzifanyia uchambuzi habari, matangazo na picha kwa usahihi ili kuhakikisha kuwa hazileti athari na pia zinaelekezwa kuwainua wanawake na kila mmoja kwenye jamii.

Raifa Ali mwanafunzi wa SUZA anayesoma tasnia ya habari, anasema muongozo huo wa sera ya jinsia utafanikisha kupambana na unyanyasaji wanaokumbana nao wanahabari wanawake.

Anasema baadhi ya wenye mamlaka katika vyombo vya habari wanaona baadhi ya kazi hazipaswi kufanywa na wanawake akitaja uandishi wa habari za uchunguzi, kutokana na mfumo dume uliojengeka katika jamii kwa kumuona mwanamke ni dhaifu.

Ofisa mwandamizi wa Baraza la Habari (MCT) Ofisi ya Zanzibar, Shifaa Said, anasema waandishi wa habari wanawake wanakumbana na unyanyasaji mkubwa kazini jambo linalowakwaza kiufanisi na wengine huacha kazi.

Anawataka kupambana na kutokuwa tayari kukaribisha unyanyasaji utakaowafanya kuwa dhaifu na duni kazini.

NAJLA BOUDEN

# Waziri Mkuu profesa, aliyetumbuliwa kwa kisa kukaribisha magumu ya IMF

•Mama wa kwanza kushika jukumu hilo Tunisia na 'ulimwengu' wa Kiarabu

**Na Gaudensia Mngumi**

MKATE ndicho chakula kikuu cha Watunisia ambacho Rais wa nchi hiyo Kais Saied, anauita mstari mwekundu, ambao hairuhusiwi kuuvuka.

Na endapo utaukanyaga ni lazima utakuwa hatarini, ndicho kilichompata Waziri Mkuu Najla Bouden, pia anayejulikana kama Najla Bouden Romdhane, ambaye kwa miaka miwili ameshika wadhifa wa Waziri Mkuu wa Tunisia.

Huyu ni mwanama wa kwanza kupewa jukumu kubwa kama hilo nchini humo pia katika eneo zima la Afrika Kaskazini, au Mangrebu.

Akizaliwa Juni 29, 1958 ni mtaalamu wa jiolojia na profesa wa chuo kikuu ambapo aliiongoza nchi hiyo kuanzia Oktoba 2021 hadi Agosti 2023. Kabla ya hapo alikuwa Waziri wa Elimu.

Septemba 2021, huku taifa hilo likiwa ndani ya mzozo wa kisiasa, Rais Kais Saied, anamtangaza Najla Bouden kuwa Waziri Mkuu na kumtaka kuunda serikali mpya ya nchi hiyo.

Tangu Saied alivunje bunge na kuanza kutawala kwa amri kabla ya kuandika upya katiba, vikosi vya usalama vimekuwa vikiwapinga mara kwa mara wapinzani wanaomtuhumu Saied kwa kuvuruga demokrasia.

Profesa Najla ni kama naye aliongoza kwa manufaa ya wazandika au wapinga demokrasia , hivyo hata naye mwezi uliopita, yamemkuta, ametumbuliwa kwenye jukumu la Waziri Mkuu, bila maelezo. Ni baada ya Rais wa Tunisia kumuonyesha mlango bila kutoa sababu na nafasi yake kuchukuliwa na Meneja Rasilimali Watu Mstaafu wa Benki Kuu ya Tunisia, Ahmed al-Hachani.

Bouden, mwanamke wa kwanza kuongoza serikali nchini Tunisia, wengi wameshangaa kuona nafasi yake inachukuliwa na al-Hachani, Mkurugenzi asiyejulikana wa zamani wa Rasilimali Watu katika Benki Kuu ya Tunisia asiye mchumi wala mtaalamu wa masuala ya siasa.



Waziri Mkuu Profesa Najla Bouden baada ya kutumbuliwa. **PICHA: MTANDAO.**

Hakuna maelezo rasmi yaliyotolewa kuhusu kutumbuliwa kwake, lakini vyombo kadhaa vya habari vya Tunisia vilivyozungumzia hatua hiyo, vilidai ni kutofurahishwa kwa Rais Saied na uhaba, hasa wa mkate ambacho ni chakula kikuu katika viwanda nchini humo hata vile vya serikali.

Serikali ya Profesa Bouden inaelezwa kuwa haikuweza kurekebisha mzozo wa kiuchumi na kijamii ambao Tunisia imetumbukia na inazidi kuzama huku rasilimali zikipungua na bei za bidhaa zikiongezeka kwa kasi ya kupaa.

"Kuna changamoto kubwa ... ili kulinda nchi yetu, dola na amani ya raia," Saied anamwambia al-Hachani baada ya kula kiapo cha kikatiba tayari kwa kazi inaripoti Al -Jazeera.

Serikali ya Bouden ilikuwa kwenye hati hati alipiga hatua kidogo katika uchumi, na hofu ilikuwa ikiongezeka kila wakati kwamba Tunisia haitaweza kulipa madeni yake ya nje na watu walipata shida kupata bidhaa za msingi kama mkate, sukari, mchele na kahawa.

'Madamu' Bouden alikuwa ameunga mkono mpango wa mageuzi ya kiuchumi ambao ungewezesha kupata mkopo wa Dola za Marekani bilioni 1. 9 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa IMF) , lakini Saied alikataa mageuzi yoyote ambayo yangehusisha kupunguza ruzuku kwenye chakula na nishati, akisema kufanya hivyo kungeweza kusababisha mvutano mkubwa wa kijamii na watu kuichukia mara dufu serikali yake.

**WATU HAWAKUSHTUKA**

Watumiaji wa mitandao ya kijamii walipokea taarifa za kufukuzwa kwa Bouden bila kujali. "Najla Bouden aliondoka kwa njia ile ile kama alivyoteuliwa," mtumiaji mmoja wa mitandao anaandika kwenye Twitter.

Kiongozi wa upinzani naye akamkejeli: "Unapoteuliwa na mapinduzi ambayo yameweka katiba pembeni pamoja na kupuuza sheria, na taasisi za serikali ya Tunisia. Tena unashirikiana na wahalifu na wauaji, basi haishangazi kuwa unabaki kuwa na simanzi kwa kutikisa kichwa. Kukufukuza kupitia mlango mdogo ni jambo la kawaida kwako," mwanasiasa wa upinzani Abdelmalik Hussein anasema kwenye ujumbe wake.

Wengine hawakukaa kimya kwa mteule wa Rais wakimwelezea kuwa al-Hachani Waziri Mkuu mpya kuwa hana sifa za kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo.

"Ni mtu alikuwa msimamizi wa idara ya rasilimali watu katika Benki Kuu ya Tunisia na hana uhusiano wowote na uchumi, mheshimiwa amestaafu kwa miaka mitano. Ana uzoefu wa aina gani?"Anahoji kwenye mtandao.

Mgogoro wa kisiasa wa Tunisia unakwenda sambamba na matatizo yake makubwa ya kiuchumi huku madeni yakiongezeka, ukuaji wa uchumi ukiyumba na kuzidi kuwa duni kwa asilimia mbili, umaskini unaongezeka na ukosefu wa ajira ukiwa juu kwa asilimia 15.

Ikikabiliwa na uchumi unaokwama, lakini pia mishahara ya chini, Tunisia tangu miaka ya 1970 imeweka ununuzi wa mahitaji muhimu kama unga, sukari, kahawa na mafuta ya kupikia kwenye mikono ya serikali lakini mambo yalipokuwa magumu vimewekwa sokoni kwa bei ya ruzuku.

Hata hivyo, kumekuwa na uhaba wa mara kwa mara wa bidhaa hizi kwa miezi ya karibuni, ukihusishwa na wafanyabiashara na wasambazaji wanaohitaji malipo ya mapema, jambo ambalo Serikali ya Tunisia imekwama na kukutana na ugumu mkubwa kulifanya.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari, Rais Saied, ambaye hivi karibuni alisema "mkate ni mstari mwekundu kwa Watunisia akimaanisha kuwa hauruhusiwi kuvukwa au kuchezewa", pale anapohofia kurudiwa kwa ghasia za ukosefu wa mkate ambazo zilisababisha vifo vya watu 150 mwaka 1984 chini ya uongozi wa Habib Bourguiba, "Baba wa Taifa la Tunisia.

**MITANDAO**

## KUREKEBISHA MKATABA WA DP WORLD, KUNAVYOWEZA KULETA KINACHOTAKIWA

**INATOKA UK. 11**

apoingia uzalendo na zinaweza kusikika kauli kama acha tupate hasara ila tuwe huru.

Utafiti huo wa 2012 unaonyesha kuwa wakati wa kutolewa usimamizi wa bandari kwa zabuni kwa ushindanishi kumezoeleka nchi za Marekani ya Kati na Kusini, siyo hivyo huko Amerika ya Kaskazini au Canada.

Sababu ni uwezo wa makundi ya wadau kama muungano wa wahudumia mizigo kampuni binafsi, kupata fedha kutoka masoko ya mitaji kujenga mageta mipya ya meli 'berths' pale inapohitajiwa.

Mifumo hiyo ya soko la fedha haiko katika nchi nyingi zinazoendelea, hivyo kutegemea wawekezaji mahsusi kuijenga, wapewe mkataba wa muda mrefu ili waweze kuingiza mtaji mkubwa. Juhudi za kufafanua vifungu vya kujitoa, na upinzani kuanzisha harakati ya kitaifa kwa jambo hili, ni kielelezo cha ugumu wa kufikia mkataba wa uendeshaji, halafu ujenzi uwe suala la ziada.

Kwa mchanganuo huo, eneo ambalo halitakuwa na ubishi kuwa linaendeshwa na kampuni kubwa ya nje ni pale wanapojenga mitambo ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa kina cha bahari kiwe na urefu wa kutosha. Kwa bandari iliyo tayari, ni kipande tu kinaweza kuwekwa chini ya kampuni ya nje bila kuzua taharuki za wenyeji, siyo kwa sababu hakuna sababu za kukodisha ila bado hazitoshi kwa wenyeji, labda kama wageni watakuwa wamelijenga eneo hilo wanalosimamia.

Ina maana kuwa malengo ya uharakishaji kushusha mizigo na kuaminiwa kwa bandari ya Dar es Salaam bado kutawezekana kwa mkataba na DP World unaolenga kutumia mifumo yao kwa uendeshaji wa shughuli kiubia na utaalum.

Maofisa wake wanaweza pia kusimamia vitengo muhimu vya uendeshaji mitambo hiyo na huku wakipanua maeneo ya bandari, au wajenge ile ya Bagamoyo kwa ajili ya kupewa mkataba mpana zaidi. Kusimamia vitengo kungefaulu zaidi endapo serikali inaamua kuuza hisa za Mamlaka ya Bandari ili iendeshwe kibiashara, au iundwe kampuni nyingine ya kusimamia bandari huku mamlaka ikiratibu ujenzi na matumizi ya bandari zote.

Wakiwa wanahisa watakuwa na uhuru au uwezo kiutendaji, si wafanywe waajiriwa wa Mamlaka ya Bandari, wakati wataalamu wao wanaweza kuiendesha, au hata wakitaka, mitambo au mifumo inayotumiwa na DP World na teknolojia.

# RC atoa siku 14 ujenzi shule ya msingi kukamilika

**Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa Shule ya Msingi Msagali ndani ya muda wa wiki mbili.

Alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara yake wilayani Mpwapwa ya kukagua miradi na miundombinu inayojengwa katika shule hiyo mpya ya Msagali inayojengwa kupitia fedha za Boost na Shule ya Sekondari Mazae kupitia fedha za serikali.

Alisema shule hiyo ilipaswa kukamilika Juni 30, 2023 na Sh. milioni 493 zimetolewa kupitia mradi wa boost kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika shule hiyo huku zaidi ya Sh. milioni 730 zimetolewa katika Shule ya Sekondari Mazae.

"Nawapatia wiki mbili hii shule iwe imekamilika hakikisheni mnachukua hatua na kuandaa mpango kazi ambao utakamilisha kazi hii kwa haraka pia vifaa vyote vinunuliwe, hapa najua pamoja na yote mnayojitetea kuna chembe chembe ya uzembe,"alionya Senyamule.

Hata hivyo, alionyesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa mabweni ya Shule ya Sekondari Mazae na kuwataka kujipanga vizuri kwa hatua zote kwa kuwa muda uliosalia wa kidato cha tano kuwasili shuleni hapo umekaribia.

"Kwenye upande wa madarasa niwapongeze, ila mabweni lazima siku zilizobaki tujipange vizuri na tuhakikishe yanakamilika kwa wakati, wapo watoto watakaotoka mikoa mbalimbali watahitaji kukaa bweni hakikisheni mnayamaliza sasa zimebaki wiki mbili tuone hamlali usingizi mfanye kazi nyingi kwa wakati mmoja ili tusimwangushe Rais Dk. Samia Suluhu Hassan," alisema na kuongeza:

"Lakini ambacho hakijanifurahisha zaidi mnaleta vifaa nusu nusu zingatieni maelekezo tunayotoa kama mkoa, mjipange vifaa ambavyo havipo hakikisheni mnavinunua,"alieleza.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwapwa, George Fuime, aliahidi kuyasimamia kikamilifu maagizo yaliyotolewa na Senyamule kwa kuongeza nguvu kazi na kupanga mpango mkakati utakaowasaidia kukamisha miradi hiyo kwa wakati.

**Lakini ambacho hakijanifurahisha zaidi mnaleta vifaa nusu nusu zingatieni maelekezo tunayotoa kama mkoa, mjipange vifaa ambavyo havipo hakikisheni mnavinunua.**

# Tembo watishia maisha wananchi Kijiji cha Muhene

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKAZI wa Kijiji cha Muheme wilayani Chamwino mkoani Dodoma wamelalamika maisha yao kuwa hatarini kutokana na kuvamiwa na tembo mara kwa mara huku wakiiangukia serikali kuwadhibiti wanyamapori hao.

Wakizungumza kijijini hapo na Nipashe, walisema tembo hao wamekuwa wakisababisha uharibifu wa makazi na chakula hali inayosababisha wakabiliwe na upungufu wa chakula.

Mmoja wa wananchi hao, Seni Masangu, alisema wanyama hao ni tatizo na wakati wa msimu wa mavuno wamekuwa wakivamia mashamba na kushambulia mazao.

**Tunaomba serikali itusaidie kudhibiti hawa tembo tumekuwa tukiishi kwa hofu siku zote.**

"Tunaomba serikali itusaidie kudhibiti hawa tembo tumekuwa tukiishi kwa hofu siku zote," alisema.

Naye Hamis Paulo, alisema tembo hao wanawakosesha amani na kuwalazimu wazazi kuwapeleka na kuwafuata shule watoto.

"Mimi kitongoji ninachoishi ni kilometa sita mtoto anatoka kule kuja kusoma hapa Muheme, sisi wazazi ikifika saa 11 jioni tupo barabarani kuwafuatilia wanafunzi na kazi zetu tunashindwa kufanya kazi za kujikwamua kiuchumi,"alisema.

Akisimulia mkasa wa tembo kuharibu makazi yake, Joshua Mathayo, alisema alivamiwa na wanyama hao nyumbani kwake mwishoni mwa mwaka jana na kuharibu nyumba na mazao yake.

Kadhalika, Saida Mwashida, alisema ndugu yake amefariki kwa kushambuliwa na tembo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Paulo Chiselu, alisema mwaka huu tembo hao wamekuwa kero na amekuwa akitoa taarifa kwa Mtendaji wa Kata ili awasiliane na maofisa maliasili.

Alisema: "Mpaka sasa kwa kweli hata sijui kama taarifa zinafika maana wananchi wangu wanapata shida na kuona kama sifuatilii."




Mkazi wa Mtaa wa Nzuguni, Mwamvula Matonya, akitafuta wateja wa kuni kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane, Kanda ya Kati jijini Dodoma jana. Mzigo mmoja wa kuni uliuzwa kwa 2,000/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bodaboda wapewa mafunzo kupunguza ajali

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

KATIKA kukabiliana na ongezeko la ajali za barabarani nchini, Chuo cha Mafunzo ya Udereva cha Wide Institute of Driving kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya ya Chamwino wameanzisha programu ya mafunzo maalum kwa madereva pikipiki zaidi ya 600.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Mkuu wa chuo hicho, Faustine Matina, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwapatia elimu madereva bodaboda ambao wamekuwa wakisababisha ajali kutokana na kukosa uelewa wa sheria za usalama barabarani.

"Lengo la mafunzo haya ni kutokana na ongezeko la ajali barabarani na bodaboda ni moja kati ya vyombo ambavyo vimekuwa vikisababisha ajali kwa wingi hali ambayo inasababisha wengi wao kupata ulemavu na wakati mwingine ajali hizo kusababisha vifo,"alisisitiza Matina.

Aidha, alisema kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabau za Serikali (CAG) ya hivi karibuni inaonyesha kumekuwa matukio mengi ya ajali nchini ambayo yanasababishwa na waendesha pikikipi maarufu kama bodaboda.

"Matukio hayo mengi yamekuwa yakisababisha vifo na ulemavu kwa baadhi yao, hivyo sisi kama chuo kwa kushirikiana na serikali ya Wilaya ya Chamwino tumeamua kuunga jitihada zinazofanywa na serikali yetu ya awamu sita kwa kutoa mafunzo haya ambapo yanalenga kuwafikia bodaboda zaidi ya 600 katika kata mbili za Buigiri na Chamwino Ikulu,"alisema.

Kadhalika, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwafikia waendesha pikipiki zaidi ya 1,800 wa wilaya ya Chamwino ili kupunguza ajali za barabarani na kuufanya usafiri huo kuwa salama kwa watumiaji.

Mkuu wa kikosi cha usalama barabarani Wilaya ya Chamwino, ASP Bwire Machunde aliwataka waendesha pikipiki kujitokeza kupata mafunzo hayo ili kujengewa uwezo wa kutambua sheria za usalama barabarani na kutambua haki zao.

"Bodaboda wote mnatakiwa kuja kupata mafunzo haya ili kusaidia kupunguza tatizo la ajali nchini baada ya mafunzo hayo kutakuwa na msako kwa watu ambao wanaendesha vyombo vyao bila kuwa na mafunzo ya usalama barabarani," alisema.

Baadhi ya bodaboda walioshiriki mafunzo hayo waliishukuru serikali kwa kuwapatia fursa hiyo ambayo inakwenda kuwasaidia kuondokana na ajali za barabarani.

Nyemo Chedego, alisema moja ya sababu ambazo zimekuwa zikichangia ongezeko la ajali nchini ni pamoja na bodaboda wengi kuendesha vyombo vya moto bila ya kuwa na mafunzo rasmi kutoka vyuo vinayotambulika.

Alisema: "Mafunzo haya kwetu yamekuja wakati mwafaka kwani watu wengi wamekuwa wakipata ajali na wengine kufa kutokaa na kutokujua sheria za usalama barabarani, hivyo mafunzo haya yatakwenda kuwa msaada kwetu kuondokana na hali hiyo."





# TIC yapiga msasa wananchi elimu ya uwekezaji nchini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI zaidi ya 500 wamenufaika na elimu ya uwekezaji inayotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa lengo la kukuza uelewa na kuongeza wawekezaji.

Aidha, kituo hicho kimepunguza thamani ya miradi inayosajiliwa kutoka thamani ya Dola za kimarekani 100,000 mpaka Dola 50,000 ili kuvutia wawekezaji wengi kujisajili na kufanya shughuli zao za uzalishaji.

Kaimu Meneja wa TIC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Deusidedit Hokororo aliyasema hayo juzi kwenye maonyesho ya kimataifa ya wakulima (Nanenane) yanayofanyika katika Uwanja wa Kimataifa wa John Mwakangale jijini Mbeya.

Alitoa taarifa hiyo wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe ambaye alitembelea banda la kituo hicho kwa lengo la kujua namna ambavyo kinawasaidia wananchi.

Hokororo alisema kituo hicho kimepunguza gharama za miradi ili kuendana na matakwa ya sheria mpya ya uwekezaji ya mwaka 2022 ambayo ilitungwa ili kuwasaidia wawekezaji wa ndani.

**Hizi ni juhudi na mipango kazi ya kituo cha uwekezaji nchini (TIC) katika kuongeza idadi ya wawekezaji wa ndani, lakini tumejipanga kutumia maonyesho haya kutoa elimu kwa zaidi ya wananchi 500 ndani na nje ya kanda ya hii.**

"Hizi ni juhudi na mipango kazi ya kituo cha uwekezaji nchini (TIC) katika kuongeza idadi ya wawekezaji wa ndani, lakini tumejipanga kutumia maonyesho haya kutoa elimu kwa zaidi ya wananchi 500 ndani na nje ya kanda ya hii," alisema Hokororo.

Alisema wataendelea kutoa elimu wa wananchi kwa kutumia njia mbalimbali baada ya maonyesho hayo kufungwa ili kuhakikisha uelewa unakuwa mkubwa zaidi na wawekezaji wanaongezeka

Alisema, kwa mujibu wa sheria hiyo ya uwekezaji wananchi ambao watawekeza na kupata cheti cha usajili kutoka TIC, watapata nafuu ya faida za kikodi na zisizo za kikodi.

Naibu Waziri Kigahe alipongeza uongozi wa TIC kwa ubunifu akisisitiza kuwa wawekezaji wa ndani wanatakiwa kusaidiwa ili wakuze mitaji yao na kuwa wachangiaji wa ukuaji wa pato la taifa.

Alisema Watanzania wengi wanashindwa kuwekeza kwenye shughuli kubwa za uwekezaji kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha na hivyo akawataka TIC kuendelea kutoa elimu hiyo ili kupanua uelewa.

Alisema wawekezaji wa ndani wanapoongezeka wanasaidia kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini na hivyo kuongeza hata ushindani kwenye soko la ndani na nje.

"Mmefanya jambo jema sana na hilo ndilo lengo la serikali yetu, tunataka wawekezaji wetu wa ndani waongezeke, lakini siyo kwamba wawekezaji wa kigeni hatuwataki tena bali tunataka tupende vya kwetu," alisema Kigahe.

Mmoja wa wawekezaji wa ndani, Christopher Mwasanguti ambaye amewekeza kwenye uchakataji wa zao la kakao wilayani Kyela alisema elimu inayotolewa na TIC ni muhimu kwa wawekezaji wazawa.

Alisema yeye kwa sasa yuko katika hatua za mwisho za kuanza uchakataji wa zao hilo kwa maelezo kuwa kampuni yake ya Levy Africa Ltd, inanunua kakao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Alisema kampuni hiyo itakuwa inazalisha tani 600 za bidhaa zitokanazo na kakao na kuziuza kwenye masoko mbalimbali ya kimataifa ambapo zaidi ya bidhaa 24 zitakuwa zinazalishwa.

Nao baadhi ya wananchi waliopata elimu hiyo kutoka kwa maofisa wa TIC walisema elimu hiyo inawasaidia kuzitambua fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo kwenye mikoa yao na namna ya kunufaika.





Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka (kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, alipotembelea banda la benki hiyo, katika maonyesho ya wakulima Nanenane jijini Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tanzania mwenyeji mkutano mifumo ya chakula Afrika

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika 2023 (AGRF) kuanzia Septemba 5 hadi 8 utakaofanyika jijini Dar es Saalam.

Mkutano huo utaisaidia kuitangaza nchi kuhusu bidhaa mbalimbali zinazotengezwa na kuongezewa thamani kupitia sekta za mifugo na uvuvi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alitoa kauli hiyo kwenye maonyesho ya kimataifa ya wakulima (Nanenane) yanayofanyika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Alisema zaidi ya washiriki 3,000 kutoka ndani na nje ya nchi watashiriki mkutano huo ambao utajadili masuala mbalimbali ikiwemo kufungua fursa za kibiashara na upatikanaji wa masoko.

"Uwepo wa mkutano huo ni sehemu ya jitihada zinazofanywa na serikali katika kuwasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi, wizara inaendelea kuhamasisha wadau wa sekta za mifugo na uvuvi kushiriki mkutano huo ili kupanua wigo wa mawasiliano ya kibiashara," alisema Ulega.

Aliongeza kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza programu mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia vijana kuendesha maisha yao kwa kuwapatia mafunzo kwa vitendo ya unenepeshaji wa mifugo na viumbe vya kwenye maji.

Alisema programu hiyo ni maono ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambapo hadi sasa zaidi ya vijana 200 wamenufaika na mafunzo hayo na sasa wanaweza kujenga mabanda na kwenda minadani na kuchagua ng'ombe wazuri, kunenepesha na hadi sasa ng'ombe 500 wameuzwa.

# Wakulima parachichi walia ukosefu wa soko

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

WAKATI serikali ikihimiza vijana na wanawake nchini kuchangamkia fursa ya kilimo cha parachichi kutokana na kuwapo kwa soko kubwa ndani na nje ya nchi, wazalishaji wa miche hiyo mkoani Iringa wanakabiliwa na changamoto ya kukosa soko baada ya kuitikia wito wa kuzalisha miche bora ya kutosha.

Wazalishaji hao wa miche ya parachichi kutoka Mafinga, ni kundi la vijana lililounda Kampuni ya Chilongola Agro Forest and Livestock Limited wamekuwa wakizalisha zaidi ya miche milioni mbili kwa mwaka lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya soko.

Akizungumza katika maonyesho ya kimataifa ya wakulima yaliyofanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, Mkurugenzi wa Kampuni ya Uzalishaji miche ya Parachichi ya Chilongola, Andrew Manfred, aliomba serikali kuunganisha na masoko ya nje ili kuuza huko.

Alisema, baada ya kutangazwa kwa fursa ya kilimo cha parachichi wao kama vijana walianzisha kundi lao la uzalishaji wa miche hiyo baada kupata mafunzo yake ndani na nje ya nchi lakini licha ya kuwa na uwezo wa kuzalishaji zaidi ya miche milioni mbili kwa mwaka bado soko ni tatizo.

"Uwezo wetu wa uzalishaji ni mkubwa sana kwa sasa tunazalisha miche bora isiyopungua milioni mbili lakini hivi navyokwambia licha ya kuuza bado tumebakiwa na miche 600,000 sasa tunaomba serikali itusaidie kupata masoko" alisema.

Akizungumzia fursa za kilimo cha parachichi, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk Geofrey Mkamilo, alisema kilimo hicho ndio kinaweza kumtoa kijana au mwanamke kwa kipindi kifupi ndani ya miaka mitatu.

Alisema, anashangazwa na vijana na wanawake wanashindwa kukichangamkia kilimo cha parachichi wakati mbegu bora za kutosha ikiwemo ya HASI ambayo matunda yake yana uwezo wa kukaa zaidi ya siku saba yasiweze kuharibika baada ya kuvunwa.

Alisema katika maonesho hayo TARI imekuja na teknolojia nyingi za mazao mbalimbali ikiwemo kilimo hicho cha parachichi ambacho katika siku za hivi karibuni soko lake la ndani na nje ya nchi limekuwa kubwa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji.

Akizungumza na wazalishaji hao wa miche ya parachichi, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alifurahishwa na vijana hao kuchangamkia fursa hiyo ya uzalishaji wa miche bora ya zao hilo kwani itawasaidia kujikwamua kimaisha.



# Wakulima kuchukua mikopo Benki ya Maendeleo Kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Maendeleo Biashara wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania Kanda ya Zanzibar, Ashura Akimu, amewataka wakulima, wafugaji na wavuvi kutumia fursa zilizopo katika benki hiyo ili kupata mikopo nafuu.

Alitoa wito huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya kilimo Nanenane eneo la Dole Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema benki hiyo imeona kuwa Zanzibar ina fursa nyingi lakini wakulima, wavuvi na wafugaji wanashindwa kupiga hatua kwa sababu ya kutokuwa na mitaji na zana za kisasa ambazo zitawawezesha kutoka katika kilimo cha kujikimu na kwenda katika kilimo biashara.

Alisema benki hiyo inatoa mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi ili kuhakikisha Zanzibar inakuwa na utoshelevu wa chakula cha kutosha na wakulima, wafugaji na wavuvi kwenda katika kilimo biashara ili kukuza uchumi wao katika ngazi ya familia na taifa.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuwasadia na kutoa mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi na pia tunawahamasisha kuja kupata elimu katika benki ili kupata fursa zilizopo.**

"Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuwasadia na kutoa mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi na pia tunawahamasisha kuja kupata elimu katika benki ili kupata fursa zilizopo," alisema.

Alisema benki hiyo mikopo yake ina masharti nafuu kwa sababu wanajali changamoto walizonazo wakulima, wafugaji na wavuvi ambao hawana hatimiliki za kuweza kudhamini mikopo yao.

Naye mtaalamu wa kilimo Zanzibar kutoka Wizara ya Kilimo, Salum Rehani, alisema ujio wa benki hiyo ni mwanga wa kufikia mafanikio kutokana na changamoto iliyopo ya upatikanaji wa mitaji katika kuendeleza kilimo kwa wakulima.

Alisema watahakikisha wanawaunganisha wakulima katika masoko ya ndani na nje ya nchi ili kupeleka mazao yao katika nchi mbalimbali ikiwemo Oman.

Alisema hivi sasa Zanzibar inauhakikia wa kusafirisha mazao ya mboga nje ya nchi yakiwa salama na tayari wana makubaliano ya kibiashara na nchi za falme za kiarabu.

Aidha, aliwataka wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwemo matunda ambayo ni adimu na hupatikana Zanzibar ikiwemo shokishoki, doriani na zambarau kwa sababu soko lake ni zuri ndani na nje nchi.

"Shokishoki hivi sasa ni zao linalosafirishwa sana katika nchi za kiarabu, hivyo ni vyema wakulima kuongeza uzalishaji," alisema mtaalamu huyo.

Asha Mshimba Jecha, kutoka katika Kijiji cha Mapapa ambaye ni mkulima alisema ujio wa benki hiyo ni faraja kubwa kwao kwa sababu kwa muda mrefu benki zilizopo zimekuwa zikiwalenga zaidi wafanyabiashara.

Alisema "Tunamatumaini kuwa benki hii itatukomboa hivyo tunaomba waliyotueleza yaende sambamba na vitendo ambayo ni kutupatia mikopo na fursa ya kutupatia mafunzo ili kuwa na wataalamu".



Ofisa Maendeleo ya Biashara wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Kanda ya Zanzibar, Ashura Akim (kushoto), akizungumza na wavuvi, wafugaji na wakulima wakati akitoa elimu kuhusu fursa zinazopatikana katika benki hiyo kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane, Dole, Wilaya ya Magharibi A Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mariam Mwinyi awahimiza wanafunzi kusoma kwa bidii

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mariam Mwinyi, amewataka wanafunzi wa shule za Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja kuongeza bidii na maarifa kwenye masomo yao ili kutoa ufaulu mzuri kwa ustawi wa maendeleo ya maisha yao ya baadae.

Mariam ambaye ni mke wa Rais wa Zanzibar aliyasema hayo katika Shule ya Kijini Sekondari Matemwe Wilaya ya Kaskazini"A" Unguja, wakati wa hafla ya kuwapa wanafunzi taulo za kike.

Alisema hakuna linaloshindikana endapo wataongeza bidii ya masomo yao ili waepukane na unyanyasaji kwenye jamii zao.

Alisema mradi wa 'Tumaini initiative' wa ZMBF unaotoa taulo za hedhi salama umelenga kufufua ndoto za wasichana na wanafunzi wa kike kuendelea kuhudhuria masomo yao bila kukatisha hata wanapokuwa katika siku zao za hedhi.

Aidha, alisema taulo hizo zitawapunguzia mzigo wa gharama za matumzi ya kila mwezi wazazi na walezi wa wanafunzi hao kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano endapo zitatunzwa vizuri pamoja na kuwaweka salama na afya njema kwasababu hazina kemikali.

Alisema mbali na kutunza afya za wasichana na wanafunzi hao lakini pia kutunza mazingira kwa kukwepa kutupa taulo ovyo badala zake wazifue na kuzitunza vizuri.

Hivyo, aliomba wafadhili zaidi kujitokeza kuufadhili mradi wa 'Tumaini initiative' ili kuwaondoshea mzigo mzito wa uchumi wanafunzi na wazazi kuepuka gharama kubwa ya kutumia taulo za kutupa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, Fatma Fungo alisema lengo la taasisi hiyo ni kuwafikia wanafunzi 20,000 ndani ya muda mfupi kwa kuwapa taulo za hedhi salama ambapo kwa kipindi cha miezi minne tayari wamewafikia wanafunzi 1,557 wa shule mbalimbali za Unguja Pemba.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Sadifa Juma Khamis, alieleza masikitiko yake ya matokeo mabaya ya Shule ya Kijini Sekondari, Matemwe.

Hivyo aliitoa wito kwa walimu na wanafunzi wa shule hiyo kuongeza jitihada ili kuibadilisha hali iliyopo sasa kwa kuleta mabadiliko makubwa na matokeo ya mitihani yao ya Taifa.

Naye, Mkurugenzi wa shule za sekondari kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Asya Iddi Issa, aliwahimiza wanafunzi hao usafi wa afya zao na mazingira wanayosomea hasa kwenye matumizi ya taulo hizo ili kupata muda mzuri wa kujisomea.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Wajamama, inayojihusisha na kutoa taaluma ya afya ya uzazi, Dk. Mwanakheir Mahmoud, alisema asilimia 48 ya wasichana na wanafunzi wa kike wanashindwa kuhudhuria masomo yao ipasavyo kila mwezi kutokana na kutokua na hedhi salama.

# Wananchi waitwa maonyesho Nanenane

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi kutembelea mabanda ya maonyesho ya Nanenane Mkoa wa Mjini Magharibi ili kuunga mkono siku maalumu ya wakulima.

Waziri Dk. Khalid aliyasema hayo alipotembelea mabanda ya maonyesho hayo ikiwa ni katika jitihada za kuwaunga mkono wakulima na kuwatia moyo katika shughuli zao za kilimo.

Akizungumza baada ya kutembelea maonyesho hayo, waziri huyo alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuyaandaa maonyesho hayo.

Pia, alipongeza uongozi wa Wizara ya Kilimo kwa kufanya kazi nzuri kwa kuweka ubunifu na vivutio vingi ambavyo vina mnasaba na ukuaji wa sekta ya utalii na uchumi wa buluu.

Aidha, Waziri Dk. Khalid alisema kuna maboresho makubwa katika maonyesho ya mwaka huu kwa kuweka vivutio mbalimbali jambo ambalo kwa vizazi vya sasa vinaweza kwenda kujifunza vitu tofauti ikiwemo masuala ya ufugaji, ujasiriamali pamoja na masuala ya utamaduni.

Katika maonesho hayo Dk. Khalid alitembelea mabanda ya wajasiarimali, wafugaji pamoja na daraja maalumu lililosanifiwa kwa ajili ya utalii.

# KILELE CHA MAONYESHO YA WAKULIMA NANENANE




Rais Samia Suluhu Hassan (katikati), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), alipokuwa akimwonyesha baadhi ya wakulima walioshika mfano wa hundi ambao ni wanufaika wa fidia ya kiasi cha fedha Dola za Kimarekani 33,537.88 sawa na Sh. milioni 85 zilizotolewa na benki hiyo kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Jubilee, baada ya tumbaku waliyolima kuathiriwa na mvua za mawe katika msimu wa kilimo uliopita, alipotembelea maonyesho ya Nanenane jijini Mbeya jana. Wa pili kushoto ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Esther Mang'enya, ambao ni wadhamini wakuu wa maonyesho ya wakulima Nanenane kitaifa mwaka huu, katika kilele chake viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Wanakikundi cha ujasiriamali kilichofadhiliwa na mgodi wa Barrick Bulyanhulu kushiriki maonyesho ya wakulima Nanenane, Kanda ya Ziwa wakionyesha bidhaa zao kwa wananchi katika viwanja vya Nyakabindi wilayani Bariadi mkoani Simiyu jana. Vikundi 11 vimewezeshwa kushiriki kwa ajili ya kutangaza bidhaa zake na kupanua mtandao wa masoko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, (katikati), akimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alipotembelea maonyesho ya wakulima Nanenane, Kanda ya Mashariki mkoani Morogoro jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela (wa pili kulia), wakiangalia bidhaa zilizoandaliwa na wakulima pamoja na wafanyabiashara katika kilele cha maonyesho ya Nanenane jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Viongozi ECOWAS kujadili hatima ya Niger kesho

**NIAMEY, Niger**

VIONGOZI wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) walipanga mkutano unaotarajiwa kufanyika kesho kujadili hatua ya serikali ya Niger kukataa amri ya kumrejesha madarakani rais aliyeondolewa na kuibua matumaini ya kimataifa ya kutafuta suluhu bila ya kutumia nguvu.

Awali ECOWAS ilitoa wito kwa viongozi wa mapinduzi ya Julai 26 kujiuzulu ifikapo Agosti sita la sivyo wakabiliwe na uwezekano wa uingiliaji wa kijeshi lakini utawala wa kijeshi badala yake ulifunga anga ya Niger na kuahidi kuilinda nchi hiyo.

Ilielezwa kuwa umoja huo haujajibu moja kwa moja licha ya kueleza kuwa kesho utafanya mkutano kwaajili ya kujadili mkwamo huo, uamuzi ambao Umoja wa Ulaya (EU) na Marekani zilisema unaruhusu nafasi ya upatanishi.

Wakati hayo yakiendelea imeelezwa kuwa kiongozi wa kijeshi nchini Niger, Jenerali Abdourahmane Tchiani, amemteua waziri wa zamani wa fedha Ali Zeine, kuhudumu katika nafasi ya waziri mkuu mpya baada ya mapinduzi.

Inaelezwa kuwa Zeine, anachukua nafasi ya Mahamadou Ouhoumoudou, ambaye alikuwa barani Ulaya wakati wa mapinduzi hayo.

Uteuzi huo umetangazwa kupitia televisheni inayomilikiwa na serikali ya Télé Sahel na msemaji wa jeshi la nchini Niger, ikielezwa kuwa Zeine amewahi kufanya kazi katika benki ya maendeleo ya Afrika nchini Chad, Ivory Coast na Gabon.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa jeshi pia limemteua Brigedia Jenerali Amadou Didilli kama mkuu wa mamlaka ya juu ya ujumuishaji wa amani nchini humo (HACP) na Brig Jenerali Abou Mahamadou kama mkaguzi mkuu wa jeshi na jeshi la kitaifa.

Vile vile, alimtaja Kanali Ibro Bachirou kuwa mkuu wa wafanyakazi wa kibinafsi wa kiongozi wa jeshi  na luteni Kanali Habibou Assoumane kama kamanda wa walinzi wa rais.

**VOA, RFI**



Wakazi wa Kijiji cha Il Ngwesi kilichopo Kaunti ya Nanyuki nchini Kenya wakiwa wameandaa bidhaa zao kwa ajili ya kuwauzia wageni. **PICHA: GWAMAKA ALIPIPI.**

# Trump atetea haki uhuru wa kujieleza

**WASHINGTON, Marekani**

WANASHERIA wa rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, kwenye kesi yake inayohusu uchaguzi wa 2020, wameitaka mahakama kutokubali ombi la upande wa mashtaka kumwekea mteja wao vizuizi vya kuzungumza.

Akitumia mtandao wake wa kijamii wa Truth Social kuelezea hali ya sasa, Trump aliandika "Sipaswi kuwekewa amri ya kuzuiliwa cha kusema kwa sababu huko kutakiuka haki yangu ya uhuru wa kusema. Badala yake, wa kuwekewa vizuizi hivyo ni Wizara ya Sheria ambayo imekuwa ikivujisha kila kitu."

Katika hati iliyowasilishwa mahakamani hapo jana, mawakili wa kiongozi huyo wa zamani wa Marekani walisema vikwazo vinavyopendekezwa na upande wa mashitaka vinakinzana na katiba ya Marekani. Mmoja wa mawakili hao, John Lauro, alisema ni ajabu kwamba kwenye kesi ambayo inahusiana na haki za kikatiba, upande wa serikali unataka mahakama kuminya haki za kikatiba.

Waendesha mashitaka walimwomba Jaji Tanya Chutkan, ambaye ndiye atakayeendesha kesi hiyo, kuwapatia amri ya kumuwekea Trump mipaka ya kipi anaweza na kipi hawezi kukiweka hadharani, baada ya rais huyo wa zamani kuandika ujumbe wa vitisho siku chache zilizopita kwenye mtandao wake kwamba watakaomuandama atawaandama.

Kwa mujibu wa waendesha mashitaka, vizuizi wanavyoviomba ni muhimu kwenye kesi hiyo kwa kuwa Trump amekuwa akitoa kauli zinazowajengea taswira mashahidi, majaji, wanasheria na wote wanaohusika na mambo ya kisheria kuwa wapo dhidi yake.

Ilielezwa kuwa upande wa mashitaka unahofia kwamba Trump anaweza kutumia mitandao ya kijamii kuchapisha nakala za mwenendo wa kesi na nyaraka nyengine za siri ambazo zinaweza kuathiri matokeo ya kesi yenyewe.

Hata hivyo, wakili wa Trump, Lauro, alisema kwamba kauli ya mteja wake haikumaanisha kitisho kwa mtu yeyote mahsusi, isipokuwa ni kauli ya jumla ambayo haipaswi kutumiwa na upande wa mashitaka kutaka kumuwekea rais huyo wa zamani vikwazo vya kutumia haki yake ya kikatiba ya kujieleza.

**DW, AFP**

## Utalii wa utamaduni unavyoondoa umaskini wanawake wa Il Ngwesi

**Na Gwamaka Alipipi, aliyekuwa Kenya**

UTAMADUNI wa kabila la Wamasai waishio Kijiji cha Il Ngwesi Jimbo la Nanyuki nchini Kenya umekuwa kivutio kwa wageni wanaofika eneo hilo kwa ajili ya kuona vivutio vya utalii ikiwamo wanyama.

Utamaduni huo licha ya kuwa kivutio lakini wanawake katika kijiji hicho wamekuwa wakipata fedha za kigeni na kuwasaidia kuendesha maisha yao.

Waandishi wa habari kutoka Kenya, Tanzania na Rwanda waliweza kufika katika kijiji hicho kwa uwezeshaji wa Shirika la Internews kujifunza masuala ya uhifadhi, kuona utamaduni wa kuvutia kutoka katika jamii hiyo inayoishi ndani ya hifadhi.

Mojawapo ya utamaduni wa kuvutia ni namna wanawake wanavyoimba nyimbo za kuwakaribisha wageni wanapofika katika eneo lao zinazoashiria amani na bahati, mchezo wa bao pamoja na nyumba zilizoezekwa kwa matope na nyasi.

Kiongozi wa jamii hiyo, Ole Polos anaeleza kwamba jamii ya maasai katika Kaunti ya Laikipia walikuwa wamoja kabla ya kutokea vita vya wenyewe kwa wenyewe na kusababisha kugawanyika, wengine wakikimbilia Tanzania.

Anasema jamii ya Maasai katika kijiji hicho wamekuwa wakinufaika na ujio wa wageni wanaofika kutembelea wanyama pamoja na vivutio vingine vilivyopo katika eneo hilo kwa kuuza vitu mbalimbali kama vikombe, shanga, nguo, vidani, na kupata fedha za kigeni.

Mmoja wa wazee katika kijiji hicho, Kimambi Legai anaeleza kuwa wakienda kuwinda wanatumia punda pamoja na mshale wenye sumu.

Anasema alipokuwa kijana akiwa mawindoni alipambana na simba na kuweza kumuua kwa kutumia kisu, japo alijeruhiwa mkononi.

Doldol anasema: "Lakini wakati wa kutega mtego vijana hawaruhusiwi. Tunashiriki sisi wazee tu kwa sababu mtego unakuwa na sumu na lazima ujaribu kama sumu inafanya kazi. Sasa vijana hawawezi hilo. Inahitaji ujasiri".

Mzee mwingine, Doldol anasema utamaduni wa kuoa ama kuolewa katika jamii hiyo unatofautiana na jamii zingine.

Anasema mwanaume ambaye ameoa wake wawili anajenga manyata mawili (makazi) na kwamba manyata ya upande wa kulia anaishi mke mkubwa na la kushoto anaishi mke mdogo.

Kuhusu michezo, Doldol anasema kijijini hapo wanacheza mchezo uitwao bao, wanacheza nyakati za jioni wakati wakisubiri chakula, kwamba wanaume pekee ndiyo wanaruhusiwa.

Anasema wachezaji wa mchezo huo huwekeana ahadi mbalimbali ikiwemo mshindi kumchukua mke au binti wa aliyeshindwa mchezo na kulala naye kwa usiku mmoja.

HABARI MICHEZO

# COASTAL YAITWANGA SINGIDA FG, ZAHERA ATAMBA ITAKUWA TISHIO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Mwinyi Zahera, amesema kikosi chake kikikaa sawa kitakuwa tishio kwenye Ligi Kuu msimu ujao kwani wachezaji wake wameonekana kumuelewa kile anachokifundisha.

Akizungumza baada ya mechi ya kujipima nguvu kati ya timu hiyo na Singida Fountain Gate, ambayo walishinda bao 1-0, Zahera raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alisema kama wameweza kupambana na timu kama Singida Fountain Gate na kuizuia, basi anaamini mambo yatakuwa mazuri msimu ujao.

Coastal iliichapa Singida Fontain Gate bao 1-0 juzi usiku katika mechi ya kujipima nguvu kwa timu zote mbili kabla ya Ligi Kuu msimu wa 2023/24, huku pia ikiwa maalum kwa ajiili ya kuzijaribu taa za Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga ambao utatumika kwenye mechi za Ngao ya Jamii zinazotarajiwa kuanza leo saa 1:00 usiku.

"Kikubwa si ushindi, ila tunajiandaa kwa ajili ya kucheza Ligi Kuu, nimewaambia wachezaji lengo ni kuangalia muunganiko wa timu kama wana mpira na wakati hawana, kushinda kwangu haikuwa kipaumbele na naona hawakucheza vibaya, wamenifurahisha kusema kweli hiyo ndiyo furaha yangu, tukiendelea hivi tutakuwa na kikosi kizuri sana cha kutishia timu zote za Ligi Kuu," alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga.

Akiwazungumzia wapinzani wao, alisema walicheza vema na kwamba kilichowatofautisha ni kwamba wao walitumia nafasi walioipata.

"Hatukuwazidi wapinzani wetu, walicheza vema wakashambulia, wakakaba vizuri, ila tulipata nafasi tukaitumia tu, ninachofurahi ni kikosi chetu kuweza kupambana na timu hiyo bora na kuwadhibiti, siyo kuwafunga," alisema.

Kocha Msaidizi wa Singida Fountain Gate, Mathias Lule, alisema timu yake ilicheza vema ila kulikuwa na makosa kadhaa yaliyofanya waadhibiwe.

"Tumecheza vizuri, kuna vitu ambavyo timu yangu imefanya vema, ila kuna sehemu tumekosea ila lengo letu kwenye hii mechi limetimia, kikubwa ni kwamba Coastal walipopata bao hawakutaka tena kutafuta lingine, wakarudi nyuma wote, hiyo ilitupa ugumu sana na wachezaji wetu hawakuweza kuwafungua ili kupata mwanya, hili tutalifanyia kazi," alisema raia huyo wa Uganda.

CHINI YA ULINZI...



Askari Kanzu akiwa amemshikilia kijana aliyekuwa amevunja sheria wakati wa mchezo wa kirafiki kati ya Simba na Power Dynamos ya Zambia kwenye Tamasha la Simba Day uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam na Simba imeshinda mabao 2-0. Kijana huyo aliingia uwanjani wakati mechi inaendelea kwenda kumkumbatia kiungo mshambuliaji wa Simba, Luis Miquissone. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## JKT Queens kambini kujiandaa CECAFA

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa, amewaasa wachezaji wa JKT Queens kuzingatia nidhamu wanapokwenda kucheza michuano ya Afrika Mashariki na Kati soka kwa upande wa wanawake (CECAFA) inayotarajiwa kufanyika Agosti 21 nchini Uganda.

Akizungumza juzi kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera alipokuwa akiikaribisha timu hiyo iliyowasili kwa ajili ya kupiga kambi, Mwasa alisema mara nyingi nidhamu ndiyo silaha kubwa kwenye michezo na kuwataka wachezaji wa timu hiyo kuitumia kama silaha ya kuwa mabingwa wanapokwenda nchini humo.

"Mara nyingi timu zetu tunaharibikiwa pale tunapofungwa goli, wengine wanakata tamaa na wengine wanashikwa na hasira. Mara nyingi hasira huwa zinasababisha kadi na hapo ndipo wachezaji wanaharibikiwa kifikra na muunganiko unakosekama, kila mtu anacheza kivyake, kwa hiyo zingatieni hilo, zingatieni nidhamu na maelekezo ya makocha na kuwa na subira ili mmalize michezo salama," alisema mkuu wa mkoa huyo.

Nao wachezaji wa timu hiyo wamemuahidi mkuu huyo wa mkoa kuwa wanakwenda kutwaa ubingwa na watarejea tena kwenye mkoa huo watakapokuwa wanatoka Uganda kwa ajili ya kumkabidhi kombe. Walimwambia kuwa wana kikosi bora ambacho kina uwezo wa kutwaa ubingwa hivyo aandae mapokezi.

JKT Queens ndiyo Mabingwa wa Tanzania Bara kwa soka upande wa wanawake walioupata msimu uliomalizika wakiinyang'anya Simba Queens iliyotwaa mara tatu mfululizo.

Hata hivyo, JKT Queens bado wana safari ndefu ili kuweza kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika kama ilivyofanya Simba Queens msimu uliopita kwani wanatakiwa wachukue Ubingwa wa CECAFA, ndiyo waweze kukata tiketi hiyo.

# Mechi za awali CAF zapelekwa Chamazi

**Na Saada Akida, Tanga**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika kwenye michezo ya hatua ya awali, watalazimika kutumia Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam baada ya dimba la Benjamin Mkapa kufungwa kwa muda kwa ajili ya ukarabati.

Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam, unafanyiwa ukarabati wa sehemu mbalimbali ikiwamo eneo la kuchezea, mabenchi ya wachezaji wa akiba, vyumba vya kubadilishia nguo na majukwaani.

Yanga wanaoiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Azam FC na Singida Fountain Gate FC Kombe la Shirikisho, watatumia Uwanja wa Azam Complex katika michezo ya awali inayotarajiwa kuanza kati ya Agosti 18 na 20, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Saidi Yakubu, alisema walipokea ugeni wa timu ya wataalam wa African Football League chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), ili kuanza ufunguzi rasmi wa mashindano hayo yanayotarajiwa kuanza Oktoba 20, 2023.

"Kikao kilihudhuriwa na viongozi wakiwamo wa serikali, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), timu ya Simba, viongozi wa ulinzi na usalama na watoa huduma mbalimbali wa uwanja huo ambao walifanya ziara ya uwanjani kuangalia ubora wa maeneo ambayo wanaenda kuyafanyia ukarabati na mahitaji yao kwa ajili ya mechi ya ufunguzi itakayofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Mashindano ya African Football League yanatarajiwa kuwa na manufaa mengi kiuchumi hapa nchini kwa kuwaleta wageni mashuhuri takriban 400 ambao watashiriki wakiwamo viongozi wa juu wa CAF na FIFA.

"Wizara tayari imeshaingia mkataba na mkandarasi Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd. (BCEG) kwa ajili ya ukarabati wa uwanja na kuanza rasmi kuanzia sasa kufanya majukumu yake," alisema Yakub.

Alisema kutokana na ukarabati huo unaotakiwa hadi Oktoba 20, mwaka huu uwe umeshakamilika, kwa sasa timu za Tanzania ambazo zimefuzu kucheza mashindano yanayoandaliwa na CAF kwa michezo ya awali wameshauriwa kutumia Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi ambao unakubalika kwenye viwango shirikisho hilo.

Yakub aliongeza kuwa ukarabati wa awali utajumuisha masuala mbalimbali ambayo CAF wanahitaji yafanyiwe kazi mapema, baadhi yanagharamiwa na serikali ikiwa ni sehemu ya mkataba na gharama zingine zinatolewa na CAF kwa ajili ya mechi hiyo ya ufunguzi ambayo itafanyika nchini.

"Michuano hiyo inashirikisha klabu nane bora Afrika, kwa upande wa Afrika Mshariki, timu ya Simba ya Tanzania ndiyo muwakilishi pekee kwenye mashindano hayo ya Afrika yanachezwa kwa mara ya kwanza kwa kushirikisha timu nane kubwa Afrika," alisema Yakubu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**ARSENAL YAMZUIA BALOGUN**

KLABU ya Arsenal imekataa ofa rasmi kutoka kwa Monaco kwa ajili ya mshambuliaji wa Marekani, Folarin Balogun, 22. **(Athletic)**

**CHELSEA YAIGUSA PSG**

CHELSEA inaripotiwa kuwa katika mazungumzo na wawakilishi wa Neymar kuhusu uwezekano wa kuhamia Stamford Bridge akitokea PSG. **(RMCSport)**

**SILVA KUONGEZA MKATABA**

KIUNGO wa kati wa Ureno, Bernardo Silva, anakaribia kuongeza mkataba wake na kubakia Manchester City, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, yuko tayari kusubiri siku chache zaidi kuona Barcelona kama itapeleka ofa ya uhamisho. **(Mundo Deportivo)**

**LAVIA ATAKIWA LIVER**

KLABU ya Liverpool italazimika kuilipa Southampton kiasi cha pauni milioni 50 kama wanataka kumpata kiungo wa kati Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 19 kutoka St Mary's. (Sky Sports)

**ANDRE APOTEZEWA LIVER**

LIVERPOOL hawajarejea tena na nia yao ya kutaka kumnunua mchezaji wa Kimataifa wa Brazil wa Fluminense, Andre mwenye umri wa miaka 22, wakati huu wakiendelea na mazungumzo na Southampton kuhusu mpango wa kumnunua Lavia. (Liverpool Echo)

Mshambuliaji wa Tottenham na England Harry Kane, 30, ataachana mpango wa kuhamia Bayern Munich ikiwa vilabu hivyo viwili havitafikia makubaliano wiki hii. **(Telegraph)**

**ALVAREZ, WEST HAM SAFI**

KLABU ya West Ham imekubali mkataba wa pauni milioni 32 kumsajili kiungo wa kati wa Ajax na Mexico, Edson Alvarez, 25. **(Guardian)**

**MOYES HAKIELEWEKI WEST HAM**

MUSTAKABALI wa Kocha wa West Ham, David Moyes, haujulikani huku kukiwa na hofu kwamba kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, anaweza kuondoka kama ataanza msimu vibaya au kama hatowaridhisha mashabiki wa timu hiyo. **(Telegraph)**

**MAGUIRE KUBAKI UNITED**

MLINZI wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30, anaweza kusalia Manchester United kwa msimu mwingine huku beki huyo wa kati akikataa kujiunga na klabu isiyoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya. **(Football transfers)**

**GORGINHO KWENDA UTURUKI**

KIUNGO wa kati wa Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 31, anaweza kuondoka Arsenal na kujiunga na klabu ya Uturuki ya Fenerbahce. **(Times)**

**ADAMS KUTUA CHELSEA**

CHELSEA inajiandaa kumnunua kiungo wa kati wa Leeds United na Marekani, Tyler Adams mwenye umri wa miaka 24, na wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo (21), kabla ya msimu huu kuanza. **(Telegraph)**

## DOND … A SOKA MAGA … ULAYA




# NEYMAR ATAKA KURUDI TENA KUITUMIKIA BARCA

Baadhi wanabishana kuunga mkono hatua hiyo na wengine - akiwamo Kocha Xavi...

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Neymar, anataka kujiunga tena na Barcelona msimu huu wa majira ya joto, lakini kuna mjadala wa ndani katika klabu kuhusu usajili wa mshambuliaji huyo, vyanzo vimeiambia ESPN.

Baadhi wanabishana kuunga mkono hatua hiyo na wengine - akiwamo Kocha Xavi Hernandez – wakiamini mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil hatafaa katika timu hiyo ya Barca.

Vyanzo vya klabu vinakataa kabisa uwezekano wa kurejea kwa mchezaji huyo wa PSG, ambaye aliondoka Barca mwaka 2017, lakini wanaonya kwamba litakuwa jambo gumu sana kifedha, na kwa sababu ya maoni tofauti juu ya kufaa kwake.

ESPN hapo awali iliripoti kwamba Neymar mwenye umri wa miaka 31, angefurahi kujiunga tena na Barcelona, na vyanzo viliongeza kwamba kwa mara nyingine ameongeza uwezekano huo katika siku za hivi karibuni.

Uwezekano wa kuhama ni mdogo, hata hivyo, kwa sababu ya matatizo ya kifedha ya klabu na upinzani wa Xavi kurejea kwake.

Zikiwa zimesalia siku nne tu Barca waanze msimu wao wa ligi wa 2023-24, wameshindwa kusajili wachezaji wao wapya - Ilkay Gündogan, Oriol Romeu na Inigo Martinez - au wachezaji ambao wameongeza mikataba yao hivi karibuni.

Kama matokeo, wana wachezaji 13 pekee wanaopatikana kwa mchezo wa Jumapili dhidi ya Getafe. Idadi hiyo inaweza kupunguzwa hadi 11 katika siku zijazo, huku Barca wakitarajia kukamilisha kuondoka kwa Franck Kessie kwenda Saudi Arabia na Ousmane Dembele kwenda PSG.

Klabu hiyo inafanya kazi kwa haraka kutatua tatizo hilo, na ujio wa Neymar utafanya hali kuwa ngumu zaidi, licha ya nia ya mchezaji huyo kuafikiana ili kufanikisha uhamisho huo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,142,1

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 09 NA 10 AGOSTI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/08/23 | 19:00 | VPS Vaasa vs Seinajoen JK | 2.91 | 3.06 | 2.27 |
| 02. 09/08/23 | 19:00 | Hodd vs Sandnes Ulf | 2.42 | 3.24 | 2.58 |
| 03. 09/08/23 | 20:00 | AEK Larnaca vs Maccabi Tel Aviv | 2.81 | 3.16 | 2.46 |
| 04. 09/08/23 | 20:30 | Chippa Utd vs TS Galaxy FC | 2.68 | 2.98 | 2.62 |
| 05. 09/08/23 | 20:30 | Polokwane City vs Stellenbosch | 3.00 | 2.95 | 2.23 |
| 06. 09/08/23 | 21:30 | Slovan Bratislava vs Maccabi Haifa | 3.13 | 3.13 | 2.22 |
| 07. 09/08/23 | 21:30 | Austria Klagenfurt vs Wolfsberger AC | 2.43 | 3.33 | 2.51 |
| 08. 09/08/23 | 22:45 | Benfica vs Porto | 2.21 | 3.17 | 3.02 |
| 09. 10/08/23 | 18:00 | FC Struga Trim Lum vs Swift Hesperange | 2.39 | 3.36 | 2.76 |
| 10. 10/08/23 | 19:00 | Omonia Nicosia vs Midtjylland | 2.59 | 3.24 | 2.59 |
| 11. 10/08/23 | 20:00 | Dila Gori vs Apoel Nicosia | 2.96 | 3.16 | 2.35 |
| 12. 10/08/23 | 20:00 | Valmiera Fk/Bjss vs Partizani Tirana | 3.06 | 3.26 | 2.24 |
| 13. 10/08/23 | 21:30 | Hibernian vs FC Luzern | 2.66 | 3.36 | 2.46 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa, vodacom m-pesa, halopesa, airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARSENAL YAKATAA OFA YA BALOGUN



**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imekataa ofa ya ufunguzi kutoka kwa Monaco kwa ajili ya mshambuliaji Folarin Balogun, lakini imekubaliana kuhusu mkataba ambao utamfanya mchezaji mwenzake wa Kimataifa wa Marekani, Matt Turner, ajiunge na Nottingham Forest, vyanzo vimeiambia ESPN.

Klabu hiyo ya Ligi Kuu England inamthaminisha Balogun kwa takriban euro milioni 58 na inafikiriwa kuwa tayari kumruhusu kuondoka kwa bei inayofaa, huku Inter Milan pia ikitarajiwa kuingia katika kinyang'anyiro cha kuwania saini yake.

Balogun amebakiza miaka miwili katika mkataba wake na Arsenal na angependelea kuhama kwa uhamisho wa kudumu ikizingatiwa uwezekano wa kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza kwenye Uwanja wa Emirates hata baada ya jeraha la goti litakalomfanya Gabriel Jesus kuwa nje ya uwanja kwa wiki chache za kwanza za msimu.

Balogun mwenye umri wa miaka 22, hakuwa sehemu ya kikosi cha siku ya mechi kilichoshinda Ngao ya Jamii Jumapili dhidi ya Manchester City kwenye Uwanja wa Wembley, baada ya kuwa nje ya uwanja kutokana na tatizo la mguu.

Balogun alicheza kwa mkopo katika Klabu ya Ligue 1 ya Reims msimu uliopita, akifunga mabao 21 katika mechi 34 alizoanza, lakini yuko nyuma ya mchezaji mpya Kai Havertz na Eddie Nketiah, ambaye anaongoza safu ya mbele ya Arsenal.

Wakati huo huo, mlinda mlango Turner anakaribia kuondoka Arsenal akiwa ameichezea klabu hiyo mara saba pekee tangu ajiunge nayo akitokea New England Revolution kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 5.75 msimu uliopita wa majira ya joto.

Turner mwenye umri wa miaka 29, atajiunga na Forest kwa dau la awali la pauni milioni saba, ambalo linaweza kupanda hadi pauni milioni 10 pamoja na nyongeza.

Kuondoka kwake kunatoa nafasi kwenye kikosi kwa ajili ya kumsajili David Raya kutoka Brentford.

Klabu hizo mbili bado hazijakubaliana juu ya ada, lakini Arsenal wana uhakika wa kufikia makubaliano chini ya bei ya Brentford ya pauni milioni 40 na mazungumzo yanayotarajiwa kuendelea wiki hii.

# Tottenham wachomoa euro mil. 100 kwa Kane

**LONDON, England**

BYERN Munich wameamua kuacha kujaribu kumsajili Harry Kane baada ya Tottenham Hotspur kukataa ofa yao ya hivi karibuni kwa nahodha huyo wa England, vyanzo vimeiambia SPN.

Vyanzo vinavyofahamu mazungumzo hayo vimependekeza kuwa ofa ya hivi punde ya Bayern ilizidi euro milioni 100 wakati nyongeza zinazohusiana na utendaji zilijumuishwa.

Bayern pia walikataa ofa Ijumaa iliyopita na wametishia kusonga mbele kwa malengo mengine ikiwa Spurs hawatakubali masharti yao.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Tottenham hawakujibu kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa na Bayern, lakini wamewafahamisha kuwa hawako tayari kukubali ofa hiyo.

Bayern wanaaminika kuwa walifanya kikao cha mkakati wa ndani Jumatatu




ambapo viongozi wakuu katika klabu hiyo wataamua iwapo wataendelea na mpango wa kumnunua Kane.

Kane mwenye umri wa miaka 30, ambaye aliifungia Tottenham mabao manne ilipoilaza Shakhtar Donetsk katika mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya Jumapili, bado hajashinikiza kuihama klabu hiyo, lakini yuko tayari kujiunga na Bayern ikiwa klabu hizo mbili zitakubaliana ada. Kane amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake ambao unamfanya kulipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki.

Licha ya vyanzo vilivyoiambia ESPN kwamba mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo hana nia ya kusaini mkataba mpya msimu huu wa majira ya joto, bado kuna matumaini ndani ya Spurs kwamba anaweza kuongeza muda wake wa kukaa ikiwa watafurahia msimu mzuri wa kwanza chini ya kocha mpya Ange Postecoglou.

## HABARI MICHEZO


32,257/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/23 | 13:00 | Daejeon Citizen FC vs FC Seoul | 2.75 | 3.20 | 2.27 |
| 02. 13/08/23 | 13:30 | Incheon United FC vs Daegu FC | 2.25 | 3.10 | 2.80 |
| 03. 13/08/23 | 14:00 | Naestved BK vs Kolding IF | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 04. 13/08/23 | 15:15 | FC Baden vs FC Vaduz | 2.65 | 3.20 | 2.33 |
| 05. 13/08/23 | 16:00 | IK Sirius vs Kalmar FF | 2.25 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 13/08/23 | 16:00 | Brentford FC vs Tottenham Hotspur | 2.70 | 3.45 | 2.37 |
| 07. 13/08/23 | 16:00 | FC Nantes vs Toulouse FC | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 13/08/23 | 16:00 | Hobro IK vs Vendsyssel FF | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 13/08/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs KRC Genk | 2.80 | 3.50 | 2.28 |
| 10. 13/08/23 | 17:00 | Motherwell FC vs Hibernian FC | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 13/08/23 | 18:00 | Burgos CF vs SD Huesca | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 12. 13/08/23 | 18:00 | FF Jaro vs HIFK Helsinki | 2.55 | 3.20 | 2.42 |
| 13. 13/08/23 | 18:30 | Halmstads BK vs IFK Norrkoping FK | 2.55 | 3.10 | 2.46 |
| 14. 13/08/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Liverpool FC | 2.70 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 13/08/23 | 19:15 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.45 | 3.30 | 2.43 |
| 16. 13/08/23 | 20:00 | Estrela Amadora vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 17. 13/08/23 | 20:30 | Albacete Balompie vs Espanyol Barcelona | 2.95 | 3.15 | 2.35 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 09/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3076 | Jeju Utd vs Pohang Steelers | 2.69 | 3.30 | 2.35 |
| 14:35 | 3648 | Shanghai Shenhua vs Shenzhen | 1.14 | 6.24 | 14.10 |
| 15:00 | 2928 | Persija Jakarta vs Pusamania Borneo | 1.99 | 3.43 | 3.18 |
| 15:00 | 3655 | Rans Nusantara vs Persepam MU | 2.32 | 3.44 | 2.58 |
| 16:00 | 1876 | Perak FA vs Penang | 4.75 | 4.04 | 1.53 |
| 16:00 | 3618 | Mamelodi Sundowns vs Kaizer Chiefs | 1.68 | 3.43 | 4.90 |
| 16:00 | 5279 | Moroka Swallows FC vs Cape Town City | 2.67 | 2.93 | 2.67 |
| 16:15 | 2579 | Gazovik Orenburg vs Sochi | 2.29 | 3.50 | 2.64 |
| 17:00 | 5238 | Pogon Siedlce vs PKS Olimpia Elblag | 2.50 | 3.16 | 2.60 |
| 18:30 | 3257 | Amazulu vs SuperSport Utd | 3.29 | 2.88 | 2.28 |
| 18:30 | 4695 | CSKA Moscow vs Fakel | 1.52 | 4.09 | 5.01 |
| 19:00 | 1079 | Fredrikstad vs Bryne | 1.58 | 3.64 | 4.96 |
| 19:00 | 1909 | Hodd vs Sandnes Ulf | 2.42 | 3.24 | 2.58 |
| 19:00 | 1982 | Malavan Bandar Anzali vs Zob Ahan | 2.76 | 2.66 | 2.76 |
| 19:00 | 2016 | Usti N Orlici vs FK Viktoria Zizkov | 6.33 | 4.39 | 1.40 |
| 19:00 | 2430 | Raufoss vs Jerv | 2.00 | 3.38 | 3.18 |
| 19:00 | 2576 | Hostoun vs Dukla Prague | 9.80 | 5.72 | 1.21 |
| 19:00 | 2598 | Ranheim vs Kongsvinger IL | 3.12 | 3.47 | 1.99 |
| 19:00 | 2691 | Gol Gohar vs Foolad Khuzestan | 2.60 | 2.75 | 2.85 |
| 19:00 | 3502 | Moss vs Kfum Oslo | 2.68 | 3.28 | 2.31 |
| 19:00 | 4016 | Aasane Fotball vs Mjondalen | 2.06 | 3.53 | 2.93 |
| 19:00 | 4262 | Persepolis FC vs Aluminium Arak | 1.92 | 3.00 | 4.07 |
| 19:00 | 4367 | SK Kosmonosy vs Varnsdorf | 7.75 | 4.89 | 1.30 |
| 19:00 | 4427 | Sogndal vs Kristiansund | 2.10 | 3.38 | 2.97 |
| 19:00 | 4491 | Young Africans vs Azam | 1.57 | 3.60 | 4.75 |
| 19:00 | 4513 | SK Otava Katovice vs Pribram | 13.20 | 5.48 | 1.19 |
| 19:00 | 5086 | FC Slovan Havlickuv Brod vs Jihlava | 10.23 | 5.53 | 1.22 |
| 19:00 | 5536 | VPS Vaasa vs Seinajoen JK | 2.91 | 3.06 | 2.27 |
| 19:00 | 5682 | IK Start vs Skeid Fotball | 1.51 | 4.25 | 4.75 |
| 20:00 | 1823 | AEK Larnaca vs Maccabi Tel Aviv | 2.89 | 3.14 | 2.40 |
| 20:00 | 3951 | RB Salzburg vs Inter | 3.82 | 3.57 | 1.79 |
| 20:00 | 5920 | Sporting Lisbon B vs Amora FC | 2.24 | 3.01 | 3.12 |
| 20:30 | 1985 | Polokwane City vs Stellenbosch | 3.08 | 3.03 | 2.29 |
| 20:30 | 2528 | Chippa Utd vs TS Galaxy FC | 2.68 | 2.98 | 2.62 |
| 20:45 | 5343 | Dinamo Moscow vs FC Krasnodar | 2.17 | 3.62 | 2.75 |
| 21:00 | 1949 | Ajax Cape Town vs Sekhukhune United | 3.02 | 3.02 | 2.34 |
| 21:00 | 3560 | KAA Gent vs Pogon Szczecin | 1.47 | 4.20 | 6.20 |
| 21:00 | 4788 | Al Hilal Riyadh vs Al Shabab Riyadh | 1.91 | 3.51 | 3.41 |
| 21:00 | 4929 | Panathinaikos vs Marseille | 3.58 | 3.28 | 1.98 |
| 21:30 | 3925 | Slovan Bratislava vs Maccabi Haifa | 3.27 | 3.17 | 2.13 |
| 21:30 | 4949 | Austria Klagenfurt vs Wolfsberger AC | 2.43 | 3.33 | 2.51 |
| 21:45 | 1402 | Bristol City vs Oxford Utd | 1.76 | 3.62 | 4.17 |
| 21:45 | 1666 | AFC Wimbledon vs Coventry | 4.37 | 3.78 | 1.69 |
| 21:45 | 3228 | Leeds vs Shrewsbury | 1.41 | 4.46 | 6.50 |
| 21:45 | 4553 | Rangers vs Servette Geneva | 1.53 | 4.03 | 5.25 |
| 21:45 | 4841 | Cardiff vs Colchester | 1.45 | 4.38 | 5.97 |
| 21:45 | 4961 | Ipswich vs Bristol Rovers | 1.49 | 4.27 | 5.56 |
| 22:00 | 4474 | Burton vs Leicester | 4.38 | 3.98 | 1.65 |
| 22:45 | 1508 | Benfica vs Porto | 2.33 | 3.14 | 2.84 |
| 23:30 | 1903 | Instituto Cordoba vs Huracan | 2.70 | 2.90 | 2.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KIBADENI AWATAKA SIMBA KUMHESHIMU ROBERTINHO

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI na kocha wa zamani wa Simba, Abdallah 'King' Kibadeni, amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kuheshimu maamuzi ya Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira, kutokana na kumtupia lawama kwa kutomchezesha straika Mzambia Patrick Phiri.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kibadeni anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao matatu 'hat-trick', kwenye mechi ya watani wa jadi 'dabi' ya Simba na Yanga, alisema mashabiki wanamkosea kocha huyo kwani kitendo cha kumlazimisha kumchezesha ni kama vile wanamuingilia kwenye majukumu yake.

"Kitendo cha wanachama na mashabiki wa Simba kumshutumu kuwa hamchezeshi Phiri ni kama kumuingilia kwenye majukumu yake, yeye ndiye anayekaa na wachezaji na anawajua nani anatakiwa kucheza mechi hii na nani asubiri acheze lini, hii kulazimika kupangwa mchezaji kwa lazima si sawasawa kabisa," alisema Kibadeni.

Mara baada ya Tamasha la Simba Day, ingawa alitambulishwa na kuonekana akipungia mashabiki kwenye orodha ya wachezaji 30, lakini hakucheza mechi hiyo, ikiwa ni mfululizo wa kutoonekana kwake uwanjani tangu msimu uliopita huku ikidaiwa kuwa ameshapona majeraha yaliyokuwa yanamkabili.

Kibadeni alisema hakuna kocha



yeyote anayeweza kumuacha mchezaji mzuri nje au kupangiwa cha kufanya kwa sababu hata yeye anahitaji ushindi kuliko mtu yeyote na timu ikipoteza wao ndiyo hubeba lawama.

"Sisi makocha timu ikifungwa ndiyo tunabeba lawama kwa hiyo hakuna anayetaka kupoteza mechi kwa ajili ya kumuweka mchezaji mzuri nje, nadhani wawe wavumilivu tu kwa sababu anachokifanya na kukiona ni sahihi kwake kwa sasa na nadhani Simba ina mashindano mengi hakuna mchezaji atakayeweza kucheza mechi zote hizo. Najua atacheza tu wasiwe na haraka," alisema kocha huyo ambaye pia alikuwa mmoja wa makocha walioifikisha Simba fainali ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) mwaka 1993 akiwa chini ya Kocha Mkuu, Muethiopia Etienne Eshete.

Wanachama na mashabiki wa klabu hiyo licha ya kumshambulia kocha huyo kwenye mitandao ya kijamii, baadhi yao wamedai huenda kocha huyo anapata shinikizo kutoka kwa baadhi ya viongozi.

Mpaka sasa hakuna kiongozi yeyote wa Simba, wala Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, aliyetaka kulizungumzia suala hilo ingawa kwenye akaunti yake yake ya instagram, baadhi ya mashabiki wamemwandikia kuwa kama kuna tatizo na mchezaji huyo walitatue haraka sana kwa sababu haileti taswira nzuri kwenye klabu.

Phiri aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu uliopita kutoka Zanaco ya Zambia, aliumia katika mechi ya Ligi Kuu Desemba 21, mwaka jana kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 na kukaa kwa muda mrefu akijiuguza.

Amecheza mechi chache hasa za Ligi ya Mabingwa akiingia kipindi cha pili kitu ambacho kinaashiria kuwa amepona, lakini amekuwa si sehemu ya kikosi cha Robertinho kwenye mechi nyingi za mwisho za Ligi Kuu msimu uliopita.

# Gamondi atoa sababu ugumu mechi Azam leo

INATOKA UK. 24

Alisema malengo yao ni kujaribu kupambania makombe yao yote waliyoyatwaa msimu uliopita na wataanza na Ngao ya Jamii leo.

"Kitu kizuri wachezaji wangu wote wapo kwenye ari nzuri, nina uwiano mzuri wa wachezaji wale watakaoanza na watakaokaa kwenye benchi, hili litanipa eneo kubwa la kuchagua nani aanze na mbinu gani nitumie kupata matokeo mazuri," alisema Gamondi.

Yanga iliwasili juzi jijini Tanga tayari kwa mchezo huo dhidi ya Azam. Msimu uliopita Yanga ikiwa chini ya Kocha Nasreddine Nabi walitwaa Ngao ya Jamii kwa kuifunga Simba mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mechi hizo za Ngao ya Jamii, ni maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2023/24, ambao unatarajiwa kuanza rasmi Agosti 15, mwaka huu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa juzi na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), siku ya ufunguzi wa ligi hiyo zitapigwa mechi tatu ambapo Ihefu FC itaikaribisha Geita Gold FC katika Uwanja wao wa Highland Estate, uliopo Mbarali mkoani Mbeya, huku Namungo FC ikiwa mwenyeji wa JKT Tanzania katika dimba la Majaliwa, lililopo Ruangwa mkoani Lindi.

Mechi nyingine itakuwa kati ya Dodoma Jiji FC itakayoikaribisha Coastal Union, wakati Azam FC ikisubiri hadi Agosti 17, kuikaribisha Kitayosce FC mchezo utakaochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. Kwa upande wa Yanga itasubiri hadi Agosti 23, mwaka huu kuvaana na KMC FC katika Uwanja wa Azam Complex.

## Robertinho, Pluijm wawaachia kazi

INATOKA UK. 24

mchezo utakuwa mzuri na mgumu pia, wachezaji wangu wamekuwa na kiwango kizuri na naamini wataonesha mchezo mzuri Alhamisi (kesho)," alisema Pluijm ambaye timu yake juzi ilicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Coast Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani na kufungwa bao 1-0.

Alisema lengo lao msimu huu ni kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita na wanataka kuanza na michuano hiyo ya Ngao ya Jamii inyohusisha timu nne za Simba, Yanga, Azam FC na wenyewe Singida Fountain Gate.

# Michezo

Jumatano Agosti 9, 2023

Nipashe




**Neymar ataka kurudi tena kuitumikia Barca** UKURASA 21

# GAMONDI ATOA SABABU UGUMU MECHI AZAM LEO

●●●Lakini ajivunia kikosi imara na kipana ambacho kinaweza kumpa matokeo wakati...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Yanga, ikishuka Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga leo kuivaa Azam FC kwenye mechi ya Ngao ya Jamii, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Miguel Gamondi, amesema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu hajawaona wapinzani wao hao wakicheza, lakini wamejiandaa kukabiliana nao kwa namna watakavyoingia uwanjani.

Mshindi wa mechi hiyo atakutana fainali na timu itakayoshinda kesho kati ya Simba na Singida Fountain Gate mchezo ambao pia utapigwa uwanjani hapo majira saa 1:00 usiku.

Akizungumza kutoka Tanga jana, Gamondi alisema kwa kiasi kikubwa wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo wa kwanza wa Ngao ya Jamii na anawaamini wachezaji wake watapata matokeo chanya.

Alisema tayari anajua kikosi chake kitakachoanza kwenye mchezo huo huku akijivunia ubora wa wachezaji wake waliouonyesha katika mechi za maandalizi.

"Tumekuwa na maandalizi mazuri sana, baada ya mchezo wetu wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Kaizer Chiefs, yapo ambayo tumeyaimarisha ndani ya kikosi, tulikuwa na maandalizi mazuri sana kule Avic Town," alisema Gamondi na kuongezea:

"Sijaiangalia sana Azam ikicheza, nafahamu walikuwa nje ya nchi kwenye maandalizi yao ya msimu, tutaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa, wachezaji wangu wanafahamu nini cha kufanya na wameonekana kuelewa vizuri mbinu zangu," alisema Gamondi.

UKURASA. 23

**KAZI KAZI!...**



Beki na nahodha msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', akiwa mazoezini na timu yake kujiandaa na mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Singida Fountain Gate itakayopigwa Uwanja wa Mkwakwani, Tanga kesho. **PICHA: SIMBA**

## Robertinho, Van Pluijm wawaachia kazi wachezaji Ngao

**Na Faustine Feliciane**

KUELEKEA kwenye mchezo wa kesho wa Ngao ya Jamii, Kocha wa Simba, Robertinho Oliviera, na wa Singida Fountain Gate FC, Hans van der Pluijm, wamesema mchezo wao wa kesho utaamuliwa na wachezaji wao kwa kuwa tayari wamemaliza maandalizi yao kwa upande wa benchi la ufundi.

Miamba hiyo itakutana katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga kesho na mshindi atakutana fainali na timu itakayoshinda leo kati ya Yanga na Azam FC.

Kocha wa Simba, Robertinho, ambaye kikosi chake kilitarajiwa kwenda Tanga jana asubuhi, amesema amepata bahati ya kuiangalia Singida Fountain Gate na amegundua ni timu nzuri iliyoimarika, hivyo anafahamu upinzani atakaokutana nao kesho.

Alisema kazi imebaki kwa wachezaji wake kuonyesha kile walichokifanyia kazi kwa muda wote wa maandalizi kuelekea mchezo huo wa kesho.

"Mchezo hautakuwa mwepesi, kila timu imejiandaa, nimewaona Singida, ni timu nzuri, lakini najivunia kuwa na wachezaji wazuri na kikosi imara, kazi imebaki kwao kuwapa furaha mashabiki wetu, tumefanya maandalizi mazuri tukiwa kambini Uturuki, pia tukiwa hapa nchini kwa siku kadhaa tumekuwa na maandalizi mazuri sana na sina hofu," alisema Robertinho.

Aidha, kocha huyo raia wa Brazil alisema wachezaji wake wapo tayari kwa mchezo huo baada ya mwishoni mwa wiki kucheza mechi yao ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Power Dynamos kwenye Tamasha la Simba Day na kufanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.

Kocha wa Singida Fountain Gate, Pluijm, akizungumza na gazeti hili jana, alisema anawaheshimu Simba kwa kuwa ni timu kubwa hapa nchini na imefanya maboresho makubwa ya kikosi chake, lakini anawaamini wachezaji wake watafanya kile walichokifanyia kazi mazoezini.

"Kwangu kazi imebaki kwa wachezaji wangu, nafahamu Simba ni timu kubwa na ina wachezaji wazuri, lakini nina timu imara,

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042